

# USALAMA KAZINI



## MWONGOZO KUHUSU USALAMA WA WANDISHI WA HABARI NCHINI KENYA

Toleo hili limechapishwa na Kenya Media Working Group

# USALAMA KAZINI



Hivos
people unlimited

CPJ

NCHRD-K National Coalition of Human Rights Defenders - Kenya

MEDIA COUNCIL OF KENYA

ARTICLE 19

KMP KENYA MEDIA PROGRAMME

TWAWEZA COMMUNICATIONS
"Working Towards a Better World"

PROTECTION international

ami African Media Initiative

© Haki ya kunakili ni ya Kenya Media Working Group, 2014

Inaruhusiwa kuiga, kunakili, kupiga chapa, kutafsiri, kutangaza, kuhawilisha, kusambaza, kutandaza ama kuendeleza taarifa hii, kwa njia yoyote au mfumo wowote, mradi tu jopo la Kenya Media Working Group litambuliwe na litajwe.

Kitabu hiki kimechapishwa nchini Kenya na Kenya Media Working Group kwa ufadhili wa Kenya Media Programme – Hivos

Agosti 2014

Kimeruwazwa na Kobole Designs Ltd.

Toleo hili limechapishwa na Print Production: Apex Printers, Nairobi

# Mawasiliano muhimu

Wandishi wa habari wanapokuwa hatarini, hali hiyo huamsha silika za kujiokoa na kwa hakika, wandishi huanza kujiuliza "Naweza kumpigia nani simu anisaidie?" Mawasiliano yafuatayo ni ya mashirika yanayopatikana kwa urahisi kwa ajili ya ushauri na, ikiwezekana, msaada wa haraka.

1. African Media Initiative, info@africanmediainitiative.org
2. Article 19, kenya@article19.org
3. Association of Media Women in Kenya, info@amwik.org
4. Committee to Protect Journalists, info@cpj.org, +254 789 758 633
5. East African Journalists Defence Network, +254 727 862 330
6. International News Safety Institute, info@newsafety.org
7. Kenya Media Programme, kmp@hivos.or.ke
8. Media Council of Kenya, info@mediacouncil.or.ke
9. National Coalition for Human Rights Defenders, info@hrdcoalition.org
10. Protection International, pi@protectioninternational.org
11. Kenya Union of Journalists, info@kujkenya.org
12. Kenya Parliamentary Journalists Association -- info@kpjake.org (254-2) 2221291
13. Community Radio Association of Kenya -- +254 722 901 422 / +254 732 542 146; Email: info@crak.co.ke
14. Twaweza Communications, info@twawezacommunications.org

# Yaliyomo

**Mawasiliano muhimu** ........ 5

## Sehemu A:

## PROTOKALI YA USALAMA NA ULINZI WA WANAHABARI NCHINI KENYA

Dibaji ........ ii
SEHEMU I: Ufafanuzi ........ iii
SEHEMU II: Mawanda ya Protokali ........ iv
SEHEMU III: Malengo ya Protokali ........ vi
SEHEMU IV: Hadhira Inayolengwa, Wajibu na Majukumu ........ vii
SEHEMU V: Mfumo wa Usalama na Ulinzi wa Wanahabari nchini Kenya ........ viii
SEHEMU VI: Matakwa ya Mwisho ........ ix
Maelezo ya Mwisho ........ ix
Kiambatisho 1 ........ xi

## Sehemu B:

## MWONGOZO KUHUSU USALAMA NA ULINZI WA WANAHABARI NCHINI KENYA

**UTANGULIZI** ........ 1

**KUHUSU MWONGOZO HUU** ........ 5

**MAMBO AMBAYO KILA MWANDISHI WA HABARI ANAPASWA KUJUA** ........ 6
Mazingira ya Sheria ........ 6

**MAANDALIZI YA MSINGI: ULINZI NA USALAMA KABLA YA KUANZA KAZI** ........ 8
Tathmini ya hatari ........ 8
Vitu Muhimu ........ 10

**KUKABILIANA NA HATARI** ........ 11

**JINSI YA KUFUATILIA AU KUKABILIANA NA VITISHO VYA**

**KUUAWA AU KUFADHAISHWA** ........ 12
Uchunguzi na Kuchunguza Wanaochunguza ........ 13
Maandamano na vurugu ........ 14

Maeneo ya ajali, moto na uokoaji ........ 15
Uhalifu Uliopangwa na Rushwa ........ 16

**MAANDALIZI YA MSINGI ........ 17**
Kuandaa mpango wa uchunguzi ........ 17
Kuwafuata wahusika wa habari wenye uhasama ........ 18
Kupata habari ........ 19
Jitihada za pamoja ........ 19
Maeneo yenye uhalifu na ugaidi ........ 20
Usafiri na vifaa vya uandishi wa habari ........ 20
Kukamatwa au kuwekwa kizuizini ........ 21
Utekaji nyara na unyang'anyi wa magari ........ 22
Vitisho vya polisi ........ 22

**MGOGORO UNAOHUSISHA GHASIA YENYE VITA ........ 26**
Kuungana au kutokuungana na wapiganaji ........ 26
Vituo vya ukaguzi ........ 28

**HATUA MAALUM KWA MWANDISHI WA HABARI MWANAMKE ........ 30**
Unyanyasaji wa kijinsia ........ 30

**USALAMA WA MAWASILIANO NA HABARI ........ 32**
Mtandao wa intaneti ........ 33

**MAMBO YA MSINGI ........ 36**
Vifaa vya utambulisho wa mwanahabari ........ 36
Maadili na usalama ........ 36
Usalama eneo la kazi ........ 37
Kufanya kazi na vyombo vya habari vya nchi za nje ........ 38
Waendesha blogu na Wanahabari Hadhira ........ 39

**WEWE NA NYUMBANI KWAKO: KUWEKA FAMILIA SALAMA ........ 40**
Mambo yako ya kiafya ........ 40
Usalama wa familia ........ 41
Baada ya majukumu/kazi. ........ 41
Njia za kujihadhari ........ 43
Kiambatanisho cha I: Kutathmini Hali ya Usalama Kabla ya Kwenda Kazini ........ 44
Kiambatisho II: Kuripoti Kisa cha Usalama na Tisho ........ 47
Kiambatisho III: Chombo cha kutathmini hatari na mikakati ya usalama ........ 48
SEHEMU YA KWANZA: Kutathmini hatari ........ 49
SEHEMU YA PILI: Mikakati ya Usalama ........ 49

**MAONI ........ 51**

# DIBAJI

Tulipokutana kwa mara ya kwanza kama jopokazi la uanahabari azma yetu kuu haikuwa kuunda mwongozo wa usalama wa wanahabari. Lengo letu lilikuwa kutathmini mazingira wanayofanyia kazi wanahabari pamoja na ulinzi na usalama wao. Ni matokeo ya Utafiti Kuhusu Usalama na Ulinzi wa Wanahabari, yaliyotupatia motisha ya kuangazia suala hili muhimu la Mwongozo wa Usalama na Ulinzi wa Wanahabari. Kupitia ufadhili wa shirika la Kenya Media Programme, ambalo ni kitengo cha shirika la kijamii kutoka Uholanzi – Hivos, hatua yetu ya kwanza ilikuwa kupiga darubini yale matokeo ya utafiti pamoja na mapendekezo. Kisha tuliangazia baadhi ya miongozo ya kimataifa kuhusu usalama wa wanahabari, na kuchanganua mambo ya kimsingi yaliyomo. Baada ya kuandika rasimu ya mwongozo, tuliandaa vikao vya kupiga msasa rasimu hiyo na tulishirikisha wawakilishi kutoka idara mbali mbali za uandishi wa habari – wakiwemo wanahabariwakala (correspondents), wanahabari , wanahabari huria (freelancers) wahariri, wamiliki wa vyombo vya habari, na miungano ya wanahabari na wahariri. Maoni tuliyopokea yalitusaidia kuboresha rasimu ya mwongozo. Tulifanya marekebisho na kuiwasilisha mbele ya jopo maalum ili iafikiwe.

Mambo yaliyomo kwenye kurasa zifuatazo ni matunda ya kazi hiyo ngumu na kujitolea kwetu. Tunafahamu kuwa bado kuna mambo fulani yanayofaa kuangaziwa kwa undani zaidi, licha kwamba juhudi zetu zililenga kushughulikia mambo husika kikamilifu. Mwongozo huu umehuishwa ili uweze kubadilishwa mara kwa mara, na kwa mujibu wa matukio katika jamii. Tumeigawa kazi hii katika sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza ni Protokali inayotoa mfumo wa mwongozo wa usalama. Aidha kuna Kauli -10 za Mkataba wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari na Mameneja, zinazotwika majukumu kadhaa ya kuhakikisha wanahabari wanafanya kazi katika mazingira salama, kuliko hali ilivyo kwa sasa. Tuna imani kuwa wale wanaojali usalama wa wafanyakazi wao watajitokeza kwa wingi na kutia saini mkataba huu, na hivyo kuthamini juhudi za walioendesha mradi huu. Sehemu ya pili ya mwongozo huu ambayo ndiyo pana, ina vigezo muhimu vinavyofaa kuzingatiwa na mwanahabari ili ajihakikishie usalama wake.

Tunashukuru kwa dhati shirika la Kenya Media Programme na Hivos, kwa ufadhili wao uliowezesha utekelezaji wa mradi huu. Pia shukrani za dhati ziwaendee wamiliki wa vyombo vya habari, wahariri na wanahabari tuliotangamana nao kwani wao ndio waliotusaidia kuipiga msasa nadharia tete na kuonyesha uhalisia wa mitazamo yetu. Tunatarajia mwongozo huu utakuwa wa manufaa na ni mchango mkubwa kwenye mtalaa wa taasisi za mafunzo ya wanahabari.

# JOPO LA MRADI

Prof. Kimani Njogu, Twaweza Communications

Wangethi Mwangi, African Media Initiative

Tom Rhodes, Committee to Protect Journalists

Ivy Kihara, Protection International, Kenya

Dr. Haron Mwangi, Media Council of Kenya

Patrick Mutahi, Article 19

Kamau Ngugi, National Coalition of Human Rights Defenders-Kenya

Kenya Media Programme - Hivos

# Sehemu A:
# PROTOKALI YA USALAMA NA ULINZI WA WANAHABARI NCHINI KENYA

# Dibaji

Sisi wadau wa vyombo vya habari nchini Kenya,

***Tukitambua*** kuwa Sura ya 4 (Sheria ya Haki) na Ibara 33, 34 na 35 za Katiba ya Kenya zinatoa hakikisho la kuwepo kwa uhuru wa kujieleza, uhuru wa vyombo vya habari, pamoja na uhuru wa kupata habari;

***Tukifahamu*** kuwa Azimio la Ulimwengu la Haki za Binadamu linajumuisha ***heshima na usalama*** wa watu wote;

***Tukielewa*** kuwa kuna masuala ya kimataifa, kitaifa na kimaeneo, hasa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu, yanayohusu ulinzi na usalama wa wanahabari;

***Tukiangazia*** malalamishi ya wanahabari kuhusu usalama wao kama inavyodhihirika kwenye ripoti iliyotolewa Aprili 2013 kwa jina "National Baseline Survey on the Safety and Protection of Kenyan Journalists";

***Tukighadhabishwa*** na kiasi kidogo cha uwekezaji katika kuhakikisha wanahabari wana usalama na ulinzi kutoka kwa vyombo vya habari na wadau wasio wanahabari kama inavyodhihirika kwenye ripoti iliyotajwa hapo juu, na tukijua kuna ripoti nyingine sawa na hiyo ya utathmini wa mataifa yote mwaka wa 2013 uliofanywa na shirika la International Women's Media Foundation (IWMF);

***Tukijua*** kuwa aghalabu uandishi wa habari huwaweka wanahabari hatarini kutokana na hila za serikali pamoja na asasi zisizokuwa za serikali, walinda usalama, makundi fisadi na wahalifu wanaowashambulia wanahabari;

***Tukijua*** kwamba Mpango wa Hatua wa Umoja wa Mataifa Kuhusu Usalama wa Wanahabari (United Nations Plan of Action for Safety of Journalists) ni dhihirisho kuwa majukumu ya wanahabari ni muhimu wakiwa kama macho ya jamii na wasambazaji wa habari, na tukijua kuwa Umoja wa Mataifa umependekeza tarehe 2 Novemba iwe Siku ya Kukomesha Kutoadhibiwa Wahalifu Dhidi ya Wanahabari;

***Tukiwa tumeshawishika kabisa*** kuwa lolote linalohujumu au kuhatarisha uhuru wa wanahabari pamoja na kazi ya wanahabari, huzuia kuwepo kwa demokrasia kwenye jamii na uimarishaji wa usalama wa wanahabari, kama ilivyo desturi ya taifa linalowezesha wanahabari kufanya kazi yao kikamilifu wakiwa macho ya jamii;

***Tukiwa tumeshawishika*** kuwa usalama wa wanahabari ni suala muhimu la haki za binadamu na ni mojawapo ya nguzo zinazowezesha kuwepo kwa haki za kujieleza;

***Tukitiwa*** moyo na jinsi usalama na ulinzi wa wanahabari unavyoangaziwa na kutetewa ulimwenguni, pamoja na juhudi za kuwezesha utekelezaji wa sera na kurasimisha mbinu za kuwahakikishia ulinzi na usalama;

***Tukitilia mkazo*** kuwepo kwa haja ya vyombo vya habari kuheshimu kanuni za uandishi wa habari wa kiwango cha juu;

***Tumekubaliana kuhusu yafuatayo***:

# SEHEMU I: Ufafanuzi

## *Mwanahabari (Journalist)*

Ni mtu aliyeajiriwa kwa kazi ya kukusanya, kutayarisha na kusambaza habari kwa sababu ya maslahi ya umma (tazama sentensi mwisho wa Protokali kwa maelezo).

## *Mwanahabariwakala (Correspondent)*

Ni mtu aliyepewa jukumu na chombo cha habari awe akikusanya habari na taarifa, kwa kandarasi fulani na malipo.

## *Mwanahabarihuria (Freelancer)*

Ni mtu anayekusanya habari bila kuwajibikia chumba chochote cha habari.

## *Mwanahabari hadhira (Citizen journalist)*

Protokali hii imetoa ufafanuzi wa jina hili kutoka kwa Profesa Jay Rosen wa Chuo Kikuu cha New York anayefafanua mwanahabari hadhira kuwa "wakati watu ambao hapo awali walikuwa hadhira wanapotumia asasi za uanahabari na kupashana habari, basi huo ni uanahabari hadhira [rejeleo: Jay Rosen. http://pressthink.org]

Hivyo basi mwanahabari hadhira ni raia aliyejitolea kukusanya habari na kuieneza habari ile kwa umma.

## *Mtetezi wa haki za binadamu*

Kwa ajili ya Protokali hii tunatumia mtazamo wa Azimio la Umoja wa Mataifa la Watetezi wa Haki za Binadamu linalorejelea "watu, makundi na miungano … inayochangia … kukomesha kabisa ukandamishaji wa haki za binadamu na uhuru wa kimsingi wa haki za binadamu, anaweza kuwa mtu yeyote au makundi ya watu wanaokuza haki za binadamu."

Kwa hivyo watetezi wanaweza kuwa raia wa kawaida, maafisa wa serikali, watumishi wa umma, wanahabari au watu walio kwenye sekta ya kibinafsi.

## *Usalama*

Usalama kwenye Protokali hii umefafanuliwa kama kutokuwepo kwa hatari au madhara yanayotokana na vitendo visivyokusudiwa kama vile ajali, matukio ya ulimwengu na magonjwa (Protection International www.protectionline.org)

## *Kutohatarishwa*

Kutotahatarishwa ni kutokuwepo kwa hatari inayotokana na vita au vitendo vilivyokusudiwa.

## *Ulinzi*

Ulinzi unamaanisha "hatua zilizochukuliwa ili kushinikiza vyombo vingine kuimarisha usalama kama vile kwa kuzuia, kuhamisha, kuficha ama usaidizi mwingine utakaopunguza madhara ya hatari" (Protection International www.protectionline.org)

## *Hatari*

Hakuna maana maalum ya hatari. Hata hivyo, kwenye Protokali hii "hatari" inamaanisha "mambo yanayoweza kutokea, hata ingawa bila kutarajiwa, na kuleta madhara". (Protection International www.protectionline.org)

# SEHEMU II: Mawanda ya Protokali

## *Ibara ya 1: Maelezo ya Jumla*

1.1 Protokali hii imetoa masharti, miongozo na maelezo kuhusu njia bora inayofaa kufuatwa na wadau wa sekta ya uanahabari katika viwango vya kitaifa na kaunti. Inanuia kutoa mfumo utakaohakikisha kuwa usalama na ulinzi wa wanahabari umezingatiwa katika sekta hii.

1.2 Protokali hii imeandikwa kwa kutumia nyaraka nyingi kama vile, Katiba ya Kenya, hasa Ibara ya 33, 34 na 35, pamoja na Sura ya 4 ya Sheria ya Haki, zote zikiwa zinahakikisha kuwa kuna uhuru wa kujieleza pamoja na haki ya umma kupata habari. Aidha, imejumuisha mambo muhimu kutoka kwa utafiti wa kitaifa wa 2013 kuhusu usalama na ulinzi wa wanahabari wa Kenya. Pia imeandikwa kuambatana na Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, Mpango wa Hatua wa Umoja wa Mataifa kuhusu Usalama wa Wanahabari na Suala la Uhalifu, na Maktaba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu.

1.3 Kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, taifa la Kenya lina jukumu kuhakikisha kuna usalama na ulinzi wa wanahabari kwani ilitia saini mapatano na makubaliano kadhaa.

1.4 Kuna mbinu za utekelezaji wa masharti haya kama inavyodhihirika kwenye kesi ya mwanahabari wa Burkinabe, Norbet Zongo, ambapo mahakama moja barani Afrika inayoshughulikia Haki za Binadamu Arusha, Tanzania, hivi majuzi ilitoa hukumu ya kusisimua kuhusu swala la uvunjaji sheria na majukumu ya serikali ya kuhakikisha wanahabari wana usalama.

1.5 Kesi ya Zongo aliyeuawa mwaka wa 1998 iliangaziwa tena baada ya harakati za kuitatua kukosa kufaulu, hali ambayo wanahabari wengi wanapitia nchini Kenya. Tangu Januari mwaka wa 2009, kesi ya mauaji ya mwanahabari wa Weekly Citizen Francis Nyaruri bado haijaamuliwa licha ya kuwa kuna ushahidi unaonyesha polisi walificha ukweli.

1.6 Imebainika kuwa wanahabari wa kike wanakumbwa na changamoto zaidi wanaporipoti, hii ikiwa ni pamoja na dhuluma za kimapenzi, kutishwa na kunajisiwa. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka wa 2013 katika mataifa yote na taasisi iitwayo International News Safety Institute, pamoja na wakfu wa International Women's Media Foundation, mara nyingi wanahabari wa kike huwa hatarini wanapofanya kazi wakiwa peke yao, huku wakiwindwa na wenzao. Kwa sababu wanadhulumiwa na wenzao ambao badala yake ndio wanafaa kuwaamini, basi dhuluma hizi mara nyingi hukosa kuripotiwa na kuadhibiwa.

1.7 Katika utafiti uliofanywa mnamo Aprili mwaka wa 2013 kuhusu wanahabari nchini, na uliofadhiliwa na shirika la Kenya Media Programme, asilimia 91 ya waliohojiwa walisema wameshuhudia utovu wa usalama wanapofanya kazi, huku nusu ya idadi hiyo wakisema wamepata vitisho vya mara kwa mara. Cha kusikitisha ni kuwa asilimia 48 ya waliotishwa waliamua kutoripoti vitisho hivyo. Walisema walikosa kuripoti kwa sababu hapo awali hakuna hatua ilichukuliwa licha ya wao kupiga ripoti baada ya kutishwa. Asilimia 29 hawakujua waripoti wapi, na wengine asilimia 23 walihisi mwajiri wao ndiye chanzo cha vitisho.

1.8 Isitoshe, chini ya mfumo wa serikali ya ugatuzi, mfumo wa uanahabari umebadilika na umehusishwa na ngazi za mashinani. Mabadiliko haya yameibua changamoto na vitisho kwa wananabari hasa katika ngazi za kaunti. Kwa mujibu wa takwimu za Baraza la Vyombo vya Habari Nchini Kenya (Media Council of Kenya), wanahabari wako kwenye hatari zaidi wakiwa sehemu zilizoko mbali na miji kwenye kaunti, ikilinganishwa na sehemu zilizo mjini. Aidha, usaidizi unaotolewa na mashirika kwa wanahabari walio kwenye kaunti (wakiwemo waandishi wakala na waandishi huria) ni mdogo ikilinganishwa na ule unaotolewa kwa wafanyakazi walioajiriwa.

1.9 Hivyo basi, kuna haja ya kuwa na mikakati ya kushughulikia changamoto zilizotajwa hapa. Hii ndio sababu Protokali hii imebuniwa.

1.10 Lengo kuu la Protokali hii ni kuhakikisha kwamba wanahabari wanafanya kazi katika mazingira salama na wanaweza kutekeleza majukumu yao kwa uwazi, huku wakiwa na uhuru wa kujieleza kwa mujibu wa katiba. Hii inawezekana kwa kufanya mambo yafuatayo:

i. Kuwa na mbinu ya kuchunguza mazingira wakati wote;

ii. Kutambua na kutathmini hatari;

iii. Kutumia mikakati inayoeleweka yenye majukumu maalum na wajibu wa kuzuia hatari;

iv. Kutekeleza sera zinazoimarisha usalama wa wanahabari;

v. Kuchukua hatua mwafaka kulinda wanahabari walio kwenye hatari; na

vi. Kuchukua hatua za dharura kushughulikia uvunjaji wa sheria kwa kuchunguza kwa kina na kuwashtaki wale wanaowavamia wanahabari.

1.11 Inatarajiwa kuwa baada ya utekelezwaji wa Protokali hii, kutakuwa na mabadiliko muhimu katika uhuru wa kujieleza na katika uanahabari kwa kupunguza vizingiti vilivyopo kwenye utendakazi wa wanahabari. Pia utekelezaji utaweza kuongeza uhuru wa wahudumu wa vyombo vya habari na kupunguza visa vya kazi yao kuingiliwa. Wakati wahudumu wa vyombo vya habari wako huru na wana ulinzi, wao huweza kukusanya, kutafiti, kuripoti na kusambaza habari muhimu inayonufaisha umma bila woga wa kudhulumiwa, kutishwa na kudhuriwa. Hivyo basi, wataweza kutekeleza majukumu yao vizuri kwa sababu watajihisi wako salama kufanya hivyo.

1.12 Protokali hii pia itachangia utendakazi wa hali ya juu na uwajibikaji kwenye sekta ya uanahabari. Vyombo vya habari vina wajibu kwa jamii. Wajibu huu ambao una mikabala miwili: maadili na utendakazi. Kwa ajili ya maadili mema, vyombo vya habari vinafaa kuwa na utendakazi wa hali ya juu na kuwa waaminifu wanapotafuta ukweli na kuripoti; wakipunguza madhara kutokea kwa kuheshimu watu wanaowapatia habari na wale wanaohusishwa kwenye habari na kukosa kuchochea; kwa kufanya kazi bila mapendeleo ya kunufaisha upande fulani bali kwa lengo la kupasha umma habari; na kuwajibikia wanaopashwa habari.

1.13 Katika utendakazi, vyombo vya habari vinatarajiwa kuandaa na

kusambaza habari inayonufaisha umma. Kwa ajili ya utendakazi wao, vyombo vya habari vina nguvu, fursa na uwezo wa kudhuru. Kwa kutambua hivi, wanahabari huwa katika nafasi ya kukosolewa na umma, wateja na wanahabari wenzao kulingana na maamuzi wanayofanya wanaposambaza habari. Vyombo vya habari vinavyozingatia usalama huwa na utendakazi wa hali ya juu na uwajibikaji kwa sababu wanahabari wana uwezo wa kutafuta habari za kweli na zinazoaminika, na kuripoti habari bila mapendeleo na hivyo kufanya umma kuwa na imani na sekta hiyo. Wanahabari wasio na usalama hawawezi kutumikia umma kikamilifu.

1.14 Aidha, Protokali hii itachangia katika kuboresha taarifa za vyombo vya habari pamoja na kuwa na mchanganyiko wa habari. Ni muhimu kuelewa kwamba wajibu mkubwa wa vyombo vya habari ni kuwa macho ya umma kwa kuangazia matukio serikalini na wanaoshikilia nyadhifa mbalimbali serikalini. Hii inamaanisha wanahabari wanatakiwa kuchunguza matukio, kuandaa taarifa na kuzisambaza kwa njia ambazo umma utaweza kufanya maamuzi kuhusu viongozi na wanajamii. Lakini uandishi wa habari kuhusu mambo tata na yanayohitaji uchunguzi wa kina, hauwezi kufanyika katika mazingira yenye hofu na ukosefu wa usalama.

1.15 Hatimaye, Protokali hii inaelezea jukumu la vyombo vya habari la kutetea uhuru zaidi na demokrasia katika jamii. Vyombo vya habari vinavyopata ulinzi hujitolea kufanya utafiti, kuripoti maovu ya viongozi katika ngazi ya kitaifa na wale wa mashinani, kuripoti utumizi mbaya wa mamlaka miongoni mwa viongozi wa kitaifa na wale wa mashinani, kuripoti ukiukaji wa haki za binadamu, kufichua ufisadi na kuwaangazia viongozi wanaotetea demokrasia na wanaowajibika. Hivyo basi, vyombo vya habari vilivyo salama ndio nguzo ya kuwepo kwa jamii yenye ufahamu na uenezaji wa maswala ya utu. Jamii yenye ufahamu ina uwezo wa kufanya maamuzi kuhusu maisha ya usoni kwa kushiriki chaguzi zilizo huru na za haki, na kwa kufanya kazi na wanahabari ili kushughulikia changamoto zinazowakumba katika siasa, uchumi, jamii, tamaduni na mazingira.

1.16 Protokali hii imeandikwa kwa njia ya kupigia upatu sera zinazohusu usalama na ulinzi wa wanahabari katika ngazi ya kaunti na ile ya kitaifa. Ni kifaa muhimu katika harakati ya kubuni sheria inayowasaidia wanahabari na utoaji wa rasilimali pamoja na kufanikisha mafunzo kwenye taasisi kuhusu masuala muhimu kama vile utathmini wa hatari, kuzuia hatari, na vyombo vya habari kujiandaa kuhakikisha usalama upo.

1.17 Wadau watatumia Protokali ili iwanufaishe kwa njia wanazotaka katika kuimarisha usalama na ulinzi wa wanahabari.

## SEHEMU III: Malengo ya Protokali

### *Ibara ya 2: Protokali hii imeandikwa kuambatana na malengo yafuatayo:*

2.1 Kutoa mwelekeo kuhusu mafunzo ya usalama na na ulinzi wa wanahabari;

2.2 Kutumika kama mwongozo wa kuhamasisha wadau wa serikali na wale wasiokuwa wa serikali kuhusu haki na majukumu ya wanahabari katika ngazi za kaunti na za kitaifa;

2.3 Kutoa mwongozo unaonuiwa kushinikiza kuwepo kwa sera ya umma kuhusu usalama na ulinzi wa wanahabari;

2.4 Kutoa mwongozo utakaowezesha ushirikiano kati ya mashirika yanayohusika na usalama na ulinzi wa wanahabari humu nchini na katika mataifa ya nje.

## SEHEMU IV: Hadhira Inayolengwa, Wajibu na Majukumu

Protokali hii inatambua vitengo vifuatavyo kama wadau wakuu na imeweka wajibu maalumu kwa kila kitengo ili kuwezesha utekelezwaji wa malengo yake. Hasa, na kama inavyopendekezwa katika Mpango wa Hatua wa Umoja wa Mataifa kuhusu usalama wa wanahabari na suala la uvunjaji sheria, serikali ina jukumu la kuimarisha usalama ili wanahabari waweze kufanya kazi yao wakiwa huru na bila kuingiliwa, pamoja na:

i) kuweka mikakati ya kisheria;

ii) kuhamasisha wahudumu wa mahakama, walinda usalama na majeshi, pamoja na wanahabari na jamii kwa jumla, kuhusu masuala ya haki za binadamu katika eneo na kimataifa na majukumu ya sheria za haki za binadamu, yanazohusu usalama wa wanahabari;

iii) Kuchunguza na kuripoti mashambulizi dhidi ya wanahabari;

iv) Kukemea mashambulizi hadharani; na

v) Kutoa usaidizi wa kutosha unaohitajika kwa kufanya uchunguzi na kushtaki washambulizi ili kukomesha uvunjaji wa sheria.

### *Ibara ya 3: Wadau wa Dola wanajumuisha:*

3.1 Serikali: Ina jukumu la kuhakikisha kuna usalama kwa jumla, kuna ulinzi na usalama wa raia.

3.2 Idara ya Polisi: Ina jukumu la kuhakikisha inafahamu vyema majukumu ya vyombo vya habari. Maafisa wa polisi wanafaa kufundishwa majukumu ya wanahabari na wahakikishe kuwa hatia dhidi ya vyombo vya habari imechunguzwa na kushtakiwa.

3.3 Mahakama: Ipate uhamasisho kuhusu maamuzi ya kesi zinazohusu vyombo vya habari na majukumu ya wanahabari.

3.4 Bunge: Wana jukumu la kutunga sheria zitakazowezesha kuwepo kwa usalama, na sekta ya uanahabari yenye utendakazi mzuri.

3.5 Kamati za Kikatiba: Zina jukumu la kuchunguza na kuhakikisha kuna utekelezaji mzuri wa katiba.

### *Ibara ya 4: Wadau Nje ya Dola:*

4.1 Mashirika ya Umma na Wasomi: Wana jukumu la kutoa uhamasisho kuhusu umuhimu wa vyombo vya habari kwa jamii na mafunzo kuhusu usalama na ulinzi wa wanahabari ili kusaidia juhudi za kampuni za vyombo vya habari. Aidha ni washirika muhimu katika kutetea haki za umma, zikiwemo zile za wanahabari.

***Ibara ya 5: Wadau wa sekta ya uanahabari wanajumuisha:***

5.1 Wanahabari: Jukumu lao la kimsingi ni kukusanya habari. Wana jukumu la kuhakikisha usalama wao, na ulinzi.

5.2 Wamiliki wa vyombo vya habari na mameneja: Kama wawekezaji, wamiliki na mameneja wa habari wana jukumu maalumu la kuhakikisha sera nzuri na mikakati madhubuti imeandaliwa ili kuwa na usalama, na ulinzi wa wahudumu wao. Hii inajumuisha kuwepo kwa mafunzo ya kutosha na usaidizi unaofaa hasa wanaporipoti matukio hatari. Aidha, inajumuisha kuchukua hatua za haraka wakati wanahabari wanatishiwa usalama wao. (Tazama Kiambatisho I)

5.3 Wahariri: Kama mameneja na watu ambao wanasimamia kazi ya wanahabari, wana jukumu la kuhakikisha wanahabari hawako hatarini. Wanafaa kutoa maelezo mwafaka na kuchukua hatua nzuri ya kuzuia hatari. Wana wajibu wa kuchunguza na kufuatilia visa vinavyotisha usalama wa wanahabari.

5.4 Asasi za kutoa mafunzo kwa vyombo vya habari: Kazi yao kubwa ni kukuza taaluma na inawalazimu kujumuisha mafunzo kuhusu usalama na ulinzi wa wanahabari kwenye mtalaa.

5.5 Mashirika ya kudhibiti vyombo vya habari: Kazi yao ni kuhakikisha kuna utendakazi wa hali ya juu kwenye uanahabari. Aidha wanahusishwa na usalama na ulinzi wa wanahabari wanapochunguza dhuluma dhidi ya vyombo vya habari.

# SEHEMU V: Mfumo wa Usalama na Ulinzi wa Wanahabari nchini Kenya

***Ibara ya 6:*** Kimsingi, mfumo huu unaangazia mambo muhimu yanayohusu mwongozo bora wa usalama na ulinzi wa wanahabari, ambao umeundwa pamoja na Protokali hii. Imetokana na uchunguzi wa 2013 wa usalama na ulinzi wa wanahabari nchini Kenya pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusu suala hilo. Marejeleo muhimu ni:

6.1 Usalama na ulinzi wa mtu binafsi.

6.2 Kutathmini hali ya hatari kabla ya kwenda kufanya kazi (*Tazama Kiambatisho II*)

6.3 Kuweka rekodi na kuripoti matukio (*Tazama Kiambatisho III*)

6.4 Kufahamu hali ya hatari na mikakati ya tahadhari kazini (*Tazama Kiambatisho IV. Chombo cha kutathmini hatari na hatua za usalama*)

6.5 Elimu ya Kimsingi kuhusu Huduma wa Kwanza.

6.6 Kutoa mafunzo kuhusu mbinu za kuripoti matukio hatari kama vile vita, uhalifu uliopangwa na ufisadi, maandamano, vurugu na hali ya taharuki, vita vinavyotokea ghafla na matukio sawa na hayo; mikasa ya ulimwengu; mikurupuko ya magonjwa; mikutano ya siasa, mechi za kandanda; vita na ukosefu wa usalama.

6.7 Kutoa mafunzo na uhamasisho kuhusu njia ya kujikinga dhidi ya vitoa machozi.

6.8 Kutoa mafunzo kuhusu njia ya kuepuka mambo yafuatayo: kutiwa mbaroni, kuwekwa kizuizini, kutekwa nyara; dhuluma za kimapenzi na njia ya kukabiliana na watu wachokozi.

6.9 Jinsi ya kufanya mahali kuwa salama.

6.10 Jinsi ya kukabiliana na walinda usalama.

6.11 Umuhimu wa orodha ya anwani za kuwasiliana na watu.

6.12 Kufahamu matukio yasiyokuwa ya kawaida kuhusu sehemu ya kazi fulani.

6.13 Mambo mengine: Maadili na usalama; wewe na nyumbani kwako, kuweka familia yako mahali penye usalama; kushughulikia vitisho.

6.14 Baada ya kazi: Kukabiliana na hatari inayoendelea kudhihirika; kukabiliana na mshtuko na mfadhaiko.

## SEHEMU VI: Matakwa ya Mwisho

### *Ibara ya 7: Usambazaji*

Protokali hii itasambazwa katika sehemu nyingi kama iwezekanavyo.

### *Ibara ya 8: Saini*

Protokali hii itakuwa wazi kutiwa saini na wadau wa vyombo vya habari na wadau wengine muhimu.

### *Ibara ya 9: Kuidhinisha*

Protokali itaidhinishwa haraka iwezekanavyo na ikabidhiwe Baraza la Kenya la Vyombo vya Habari.

### *Ibara ya 10: Kuhifadhiwa*

Protokali itahifadhiwa na Barazala Kenya la Vyombo vya Habari.

### *Ibara ya 11: Kutekelezwa*

Protokali hii itaanza kutumika punde tu baada ya kuidhinishwa.

### *Ibara ya 12: Uchunguzi na Utekelezaji*

Baraza la Kenya la Vyombo vya Habari litaendesha uchunguzi na kufuatilia mambo yaliyotajwa kwenye Protokali hii kwa ushirikano wa karibu na Kituo cha Mkakati wa Usalama wa Vyombo vya Habari (Strategy Centre for Media Safety), pamoja na mashirika mengine ya wadau. Chombo maalumu cha ufuatiliaji kitaundwa kwa kazi hii.

### *Ibara ya 13: Marekebisho*

Protokali hii imeundwa kama kitu chenye uhai na hivyo itakuwa ikibadilika mara kwa mara ili iambatane na hali iliyoko. Mabadiliko yoyote yatakayopendekezwa yatatumwa kwa mhifadhi ambaye atashirikiana na Kituo cha Mkakati wa Usalama wa Vyombo vya Habari (Strategy Centre for Media Safety) na wadau wengine kufanya marekebisho.

## Maelezo ya Mwisho

*Je, mwanahabari ni nani?* Siku za nyuma, mwanahabari alifafanuliwa kuwa mtu aliyeajiriwa na chumba cha habari ili akusanye habari, aiandike na aisambaze kwa umma. Sasa, mtandao umeleta mabadiliko ya jinsi habari inasambazwa, na mwanahabari ameacha kuelezewa kuwa mtu ambaye kazi yake kama mwajiriwa ni

kukusanya, kuandika na kusambaza habari pekee. Hivyo basi, jamii imeanza kuwa na ufafanuzi mpana, ambapo kinachoangaziwa ni majukumu ya wanahabari na sio tu watu wanaofanya kazi katika vyombo vya habari. Mfano mzuri ni Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu (United Nations Human Rights Committee) inayofanya uanahabari kuwa, "ni jukumu linalotekelezwa na vitengo vingi, wakiwemo maripota walioajiriwa na wachanganuzi, pamoja na waandishi kwenye mtandao na watu wengine wanaojihusisha na uchapishaji katika magazeti, kwenye mtandao au kwingineko." [maelezo ya jumla nambari 34 kwenye Ibara ya 19 ya Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Raia na Haki za Siasa].

Kwa upande mwingine, kuna ufafanuzi unaotolewa na Baraza la Kenya la Vyombo vya Habari. Lakini Baraza hili limeenda kinyume na limeeleza mwanahabari kuwa "*mtu yeyote mwenye stashahada au shahada ya somo la uanahabari kutoka taasisi ya elimu ya juu inayotambulika na Baraza la Vyombo vya Habari; au mtu yeyote aliyekuwa akifanya kazi ya uanahabari kabla ya utekelezaji wa Sheria ya Vyombo vya Habari ya mwaka wa 2013 nchini Kenya (Kenya Media Act 2013), ambaye amehitimu kwa kiwango tofauti na kile kinachotambuliwa na Baraza; mtu anayepata riziki kutoka kwa uanahabari, au mtu yeyote ambaye mara kwa mara anajihusisha na shughuli za uanahabari na Baraza linatambua hivyo*".

Changamoto iliyoko ni namna ya kuainisha mitazamo hii miwili. Cha muhimu ni kuwa ufafanuzi huu wa Baraza la Kenya la Vyombo vya Habari umetoa nafasi kubwa ya kujumuisha wadau wengine.

Kwa sababu hii Protokali inahusu usalama na ulinzi wa wanahabari, ni muhimu kusisitiza kuwa inalenga wahudumu wa chumba cha habari, iwe wameajiriwa au wanapata marupurupu, na wanaotegemea kusaidiwa na waajiri wao, meneja, mkandarasi au msimamizi, kwa masuala ya usalama na ulinzi.

Kwa upande mwingine, na tofauti na wanahabari hadhira au watu wanaojieleza kupitia aina tofauti ya vyombo vya habari, kundi hili linajumuisha wadau wa vyombo vya habari ambao wanahudumia afisi kuu, inayoshughulikia usalama wao.

Tunahisi kwamba suala lingine muhimu linalofaa kuzingatiwa ni kanuni ya *maslahi ya umma* katika uanahabari. Suala hili ni muhimu kwani inatenganisha vitendo vya wanahabari vya maslahi ya binafsi na "uanahabari wa kitaaluma." Kimsingi, hii ndiyo tofauti baina ya ya uanahabari uliojikita katijka maadili na uanahabari na utanzu wa simulizi unaendeshwa na "wanahabari hadhira."

Kwa sababu ya Protokali hii, tumeshawishika kuwa ufafanuzi wowote ule unafaa kuleta pamoja mambo ya siku za nyuma na ya kisasa, huku ukiepuka kutoa taswira kwamba uanahabari ni jambo lililowazi kwa kila mtu na lisilokuwa na masharti au yenye kunufaisha jamii.

Kwa hivyo basi, maana ya neno mwanahabari "*kuwa ni mtu aliyeajiriwa kwa kazi ya kukusanya, kutayarisha na kusambaza habari kwa sababu ya maslahi ya umma*" inaonekana kuwa bora. Ni ufafanuzi uliotolewa na wakili wa vyombo vya habari ambaye pia ni mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dayton, Profesa Jonathan Peters, wakiwa na Edson C. Tandoc Jr. wa Shule ya Wanahabari ya Missouri, katika mjadala wa Shield Law nchini Marekani. Tazama jinsi ufafanuzi huo ulivyoepuka suala la viwango vya elimu, masomo au jambo kama hilo.

# Kiambatisho 1

## *Kauli 10 za mkataba wa wamiliki wa vyombo vya habari, mameneja na wahariri kuhakikisha usalama wa wandishi wa habari*

Dola, wawekezaji wa vyombo vya habari, wamiliki, waajiri, mameneja na wahariri wana wajibu mkubwa kuhakikisha kuwa uhuru wa kujieleza umelindwa na kwana wanahabari wako salama na wamelindwa. Kwa hivyo ni wajibu wao kuwezesha kuwepo kwa mazingira salama na yanayowawezesha wanahabari kufanya kazi yao. Hili ndiko lengo la Mpango wa Hatua ya Umoja wa Mataifa Kuhusu Usalama wa Wanahabari pamoja na suala la Uhalifu Usioadhibiwa.

Ni sababu hii wanatakiwa kuunda vitengo vya usalama katika vyumba vya habari ili watekeleze, wachunguze na wahakikishe mambo ni shwari kama ilivyoandikwa kwenye amri hizi.

1. Kutathmini na kuelewa kiwango cha hatari na kuhakikisha mwanahabari anaelewa kikamilifu, kumpatia mwongozo wa jinsi matukio yanaripotiwa na kumpatia nafasi ya kukubali au kukataa.

2. Wanahabari wanaoripoti matukio hatari wanafaa kuelimishwa kuhusu mazingira yasiyokuwa na usalama, na kufunzwa kutoa Huduma ya Kwanza, hatua za kimsingi zinazofaa kufuatwa pamoja na usaidizi wa kisaikolojia.

3. Kutoa ushauri wa mara kwa mara pamoja na mafunzo kuhusu tukio analoenda kuripoti.

4. Kata bima ya wanahabari itakayofidia majeraha, kifo, mali na vifaa vya kazi.

5. Toa usaidizi wa kisheria dhidi ya kushtakiwa mahakamani ili kukomesha uhalifu.

6. Toa usaidizi unaohitajika na wanahabari wanapoenda kuripoti matukio kama vile usafiri, vifaa vya kujilinda na fedha.

7. Weka wanahabari katika hali nzuri, pamoja na kutoa ushauri nasaha hasa baada ya kuripoti matukio yanayotamausha.

8. Weka mkakati mwafaka wa usalama, pamoja na mkakati wa kuwasaidia na kuwalinda wanahabari kama vile kuwa na mpango wa kuwaondoa au kuwahamisha wanahabari na kuwa na meneja wa usalama wa kampuni.


9. Kuanzisha hazina itakayoshughulikia usalama wa wanahabari walio mashinani na waleta habari waliopewa majukumu maalumu. Hazina itafadhiliwa kupitia ukusanyaji wa kodi wa kila mwaka kutoka vyumba vyote vya habari pamoja na/au mapato ya Baraza la Vyombo vya Habari, yanayotokana na faini zinazotozwa Vyombo ya Habari na wandishi wa habari wanaokosa.

10. Kuweka mikakati maalumu ya kushughulikia masuala ya jinsia na utamaduni kama vile dhuluma za kimapenzi.

# Sehemu B:

# MWONGOZO KUHUSU USALAMA NA ULINZI WA WANAHABARI NCHINI KENYA





# UTANGULIZI

Katiba ya Kenya iliyotangazwa mnamo Agosti 2010 inathamini mambo mengi. Miongoni mwa hayo, katika Sura ya 4 ya Sheria ya Haki Ibara za 33, 34, na 35 uhuru wa mtu kujieleza, uhuru wa vyombo vya habari na kupata habari, na uhuru wa kupata habari umelindwa. Katika Ibara ya 33, Katiba imetoa uhuru wa mtu kutafuta, kupokea au kutoa habari au dhana; uhuru wa sanaa; uhuru wa kitaaluma na uhuru wa utafiti wa kisayansi. Uhuru wa vyombo vya habari unalindwa na Ibara ya 34. Ibara hiyo inatoa uhuru na kutoingiliwa kwa vyombo vya habari vya aina ya redio, magazeti,




majarida, televisheni, filamu, video, mtandao wa kompyuta na mengineyo.

Dola imezuiliwa isidhibiti kumuingilia mtu yeyote anayefanya kazi ya utangazaji, utengenezaji au usambazaji wa machapisho yoyote, au uenezaji wa habari kwa kutumia njia yoyote. Katika Ibara ya 34 (5), kuna matarajio ya kuwa na chombo huria kitakachotunga na kusimamia sheria za vyombo vya habari. Chombo hicho hakitakuwa chini ya udhibiti wa serikali, ama maslahi ya kisiasa au kibiashara.

Katika Ibara ya 35, Katiba inalinda haki ya kila mwananchi ya kupata habari iliyohifadhiwa na Dola, pamoja na habari iliyohifadhiwa na mtu binafsi na inayohitajika kwa ajili ya kutekeleza au kulinda haki au uhuru wa msingi. Haki hizi zina maana ya msingi katika sekta ya utangazaji.

Katiba inafafanua zaidi kuhusu mfumo wa Serikali ya Ugatuzi, ambao iwapo utatekelezwa vizuri, utawezesha umma kushiriki ipasavyo katika utawala, kuwajibishwa kwa viongozi na kuongezeka kwa nafasi ya vyombo vya habari huria vyenye wandishi wa habari katika jamii wakiwa mstari wa mbele katika kuongeza wigo wa habari.

Pamoja na kuwepo kwa mfumo wa sheria, uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari nchini Kenya bado unatishiwa. Usalama wa wandishi wa habari unaendelea kutishiwa. Kuna kesi nyingi za kushambuliwa, kutiwa mbaroni

na kufadhaishwa, ambazo zinaonyesha kutoheshimu uhuru wa kujieleza. Kadhalika, mashambulio dhidi ya wandishi hadhira, uchunguzi wa taarifa katika mtandao wa kompyuta wenye shinikizo la kisiasa na sheria zinazokandamiza mawasiliano katika mtandao wa kompyuta ni baadhi ya vitu vinavyoibuka na kutishia uhuru wa mawasiliano kupitia mtandao nchini Kenya.

Katika utafiti msingi ulioendeshwa Disemba 2012 na Kenya Media Working Group, ziada ya asilimia 70 ya waliohojiwa walisema hawaridhishwi na viwango vya hatua za usalama vilivyopo katika vituo vyao vya habari. Kinachojitokeza zaidi ni kwamba zaidi ya nusu ya waliohojiwa walikuwa na mtazamo kwamba vituo vya habari vinajali zaidi usalama wa vifaa vya utangazaji na majengo kuliko usalama wa wafanyakazi.

Kadhalika, hao wandishi wa habari walikuwa na mtazamo kwamba vituo vya habari havina nia na madhumuni ya kuchunguza uhalifu unaofanywa dhidi ya wafanyakazi wao. Wanasema ni kazi bure kutegemea mamlaka husika kuchunguza mashambulizi dhidi ya wandishi wa habari hasa wahusika wakiwa wafanyakazi wa serikali. Zaidi ya hayo, kutokana na matokeo ya huo utafiti, vyama vya vyombo vya habari na Umoja wa Wandishi wa Habari wa Kenya (*Kenya Union of Journalists*) havikuwa na uwezo uliotakiwa kuweza kuwalinda wandishi wa habari.

Fauka ya hayo, kwa kweli, na kulingana na viwango vya dunia, mazingira ya kazi nchini Kenya bado ni salama kwa wandishi wa habari. Kwa mfano, tofauti na jirani yake Somalia, Kenya haijawahi kuwekwa katika orodha ya nchi hatari zaidi kwa wandishi wa habari. Orodha hii hutolewa mara kwa mara na mashirika ya habari yasiyo ya kiserikali kama Kamati ya Kuwalinda Wandishi wa Habari (Committee to Protect Journalists), Ibara ya 19, Wandishi wa habari Wasio na Mipaka (Reporters Without Borders), Freedom House, Shirikisho la Kimataifa la Wandishi wa Habari (International Federation of Journalists), na Taasisi ya Kimataifa ya Wandishi wa Habari (International Press Institute).

Ikilinganishwa na mataifa hayo, Kenya hufikiriwa kuwa na mazingira salama kwa wandishi wa habari. Kati ya vifo 609 vya wandishi wa habari vilivyotajwa na PEC katika kipindi cha miaka mitano (ambayo ni sawa na mwandishi wa habari mmoja kuuawa kila baada ya siku ya tatu kwa ajili ya kutoka nje ya nyumba yake kutimiza wajibu wake kwa maslahi ya umma), kesi nne zilitokea Kenya. Kesi hizo zinawahusu Trent Keegan, raia wa New Zealand aliyekuwa mpiga picha wa magazeti ya Ireland na New Zealand (Mei 28, 2008); Francis Nyaruri, mwandishi wa habari wa gazeti la Weekly Citizen (Jan 29, 2009), Bernard Wesonga wa gazeti la The Star huko Mombasa, Machi 21, 2013, na Rulhila Adalia-Sood wa Kiss TV, East FM, Septemba 21, 2013 - wakati wa mashambulizi ya kigaidi katika Westgate

## Kenya bado ni salama kwa wandishi wa habari

Mall. Ni muhimu kufahamu hapa kwamba, kulingana na CPJ, wakati mwingine sababu ya mauaji huwa haijulikani ama hakuna uhakika.

Hata hivyo, itakuwa ni makosa kutumia mauaji kama kipimo pekee cha kuwepo au kutokuwepo kwa usalama katika mazingira ya kazi ya wandishi wa habari. Katika Viashiria vya Maendeleo ya Vyombo vya Habari: mfumo wa kutathmini maendeleo ya vyombo vya habari (Media Development Indicators (MDI): *A framework for assessing media development*[1]), UNESCO inabainisha vigezo muhimu vifuatavyo:

- Vitisho, unyanyasaji au ufuatiliaji wa wandishi wa habari na wafanyakazi wa vyombo vya habari.
- Mashambulizi ya kimwili, kuwekwa mahabusu kinyume cha sheria, au kutishwa kutokana na kufanya shughuli zao halali.
- Kufungwa kwa vyombo vya habari kwa kuendesha shughuli zao halali, au vitisho vya kufungiwa.
- Kuwepo kwa kwa ushahidi wa mazingira ya ukatili.
- Ukosefu wa sera katika mashirika ya habari kwa ajili ya kulinda afya na usalama wa wafanyakazi wao na wafanyakazi huria.
- Ukosefu wa hatua za hifadhi ya jamii kwa wafanyakazi wote, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wa muda na wafanyakazi huria.
- Wandishi wa habari kuwa na utaratibu wa wanahabari kujidhibiti mara kwa mara wa habari kutokana na hofu ya adhabu, unyanyasaji au kushambuliwa.
- Ukosefu wa ulinzi wa kisheria na kutoheshimu usiri wa vyanzo vya habari

Mtu anaweza kuongeza kwamba, kuna mwenendo wa tabaka la wanasiasa kuhakiri, kukemea na kulaani vyombo vya habari na wandishi wa habari pindi wanapowawajibisha hao viongozi kutokana kwa ulafi wao, na mwenendo wa kukataa kutoa msaada wa matangazo kwa vituo vya usambazaji wa habari ambavyo hufikiriwa kuwa vinaikosoa sana serikali. Kwa kutunga sheria mbili za vyombo vya habari zenye utata mwaka 2013 – Sheria ya Kenya ya Habari na Mawasiliano (Marekebisho) na Sheria ya Baraza la Habari - bunge hakika liliiwezesha Serikali kudhibiti vyombo vya habari kwa kuipa serikali mamlaka ya usimamizi juu yao, na kujenga hofu miongoni mwa wandishi wa habari na vyombo vya habari ambavyo viko hatarini kutozwa faini kwa kuripoti juu ya masuala yenye utata, kama vile ufisadi na uwajibikaji.

Taswira ya Kenya inafifia pale ambapo baadhi ya viashiria hivi vinatumika kama vigezo vya mazingira ya kazi ya wandishi wa habari. Katika mazingira kama hayo hali ya watu binafsi na kampuni kujithidhibiti inaendelea kustawi, pamoja na kulazimika kupunguza kasi ya uchunguzi wa habari nyeti kwa kuhofia maisha yao na kuepuka kupoteza msaada wa matangazo, hususan kutoka kwa idara za serikali. Hii ina athari ya kuingilia uhuru wa kihariri, kudhoofisha uandishi wa habari kwa maslahi ya umma, kupunguza usambazaji wa habari bila vikwazo na kuwekea vikwazo uwezo wa wananchi kufanya maamuzi muhimu pale inapohitajika.

4. Mbinu ya kipekee ya kuchunguza na kubainisha mazingira ya uandishi wa habari katika nchi na kuonyesha mapungufu katika maendeleo ya uandishi wa habari. Kipengele kimoja kifupi katika hivi viashiria kilihusika na masuala ya usalama wa wandishi wa habari (aya 3: 13 na 3:14). www.unesco.org/images/0016/001631/163102e.pdf

# KUHUSU MWONGOZO HUU

Madhumuni ya mwongozo huu ni kuwapa wandishi na vyombo vya habari maarifa ya ziada (vidokezo) na baadhi ya zana ambazo zinaweza kuwa na manufaa katika kuboresha ulinzi na usalama wao. Hii ni miongozo muhimu kwa ajili ya ulinzi na usalama kwa ujumla, na inatarajiwa kwamba kutumika kwao nchini Kenya, kutapelekea kuweka mazingira ya kazi yaliyo salama kwa wandishi wa habari. Hatimaye, usalama ni jukumu la kila mtu na sote tuna wajibu wa kuwalinda wengine na kujilinda wenyewe.

Mwongozo ni ishara ya kuwa na mwelekeo mpya katika uendeshaji wa kazi ya uandishi wa habari. Kwa kiasi kikubwa mwongozo huu umenufaishwa na miongozo mingine inayotumika duniani pamoja na ujuzi wa wanataaluma wa uandishi wa habari wa ndani ya nchi. Mwongozo huu unaongozwa na ukweli kwamba kuwepo kwa vitisho au mashambulizi dhidi ya wandishi wa habari siyo hali inayotokea katika eneo moja tu duniani, bali kuna tofauti baina ya maeneo yote katika idadi na makali ya hayo matukio. Hivyo, miongozo ya aina hii huwa inafana katika muundo, maudhui, mtazamo na msukumo.

Mwongozo huu unajaribu kutoa muktadha wa nchini ili kuweza kushughulikia mambo ambayo yanahusu mazingira ya kipekee ya Kenya. Ingawa hatua za dhati zimechukuliwa ili kuufanya huu mwongozo uwe wa kina, kuna uwezekano kwamba mwongozo haujaweza kuzingatia hatari au athari zote. Kwa hivyo, kuna fursa ya kufanya utafiti zaidi ili kuimarisha hati hii.

Cha kuchangia zaidi mwongozo huu ni Protokali ya Usalama na Ulinzi wa wanahabari nchini Kenya inayofafanua wajibu na majukumu ya wadau muhimu katika sekta ya uandishi wa habari.

# MAMBO AMBAYO KILA MWANDISHI WA HABARI ANAPASWA KUJUA

## Mazingira ya Sheria

Mbali na mafunzo ya taaluma yao, wandishi wa habari wa Kenya wanapaswa kuelewa mfumo wa kisheria unaoongoza kazi zao. Hii ina maana kutumia muda wao na nguvu zao kuzifahamu sheria, sera na mikataba inayohusiana na uhuru wa habari na kutoa maoni au kujieleza, usalama na ulinzi wa wandishi wa habari pamoja na ueledi na maadili katika kuripoti habari. Hiyo ndiyo inawapa wandishi wa habari ulinzi kamili chini ya sheria za ndani na za kimataifa, na kuiwajibisha Serikali na waajiri kuwekeza katika usalama wao. Yafuatayo ni baadhi ya nyaraka zilizopendekezwa:

a) Katiba ya Kenya (2010): www.kenyalaw.org/Downloads/TheConstitutionKenya.pdf


b) Azimio La Haki za Binadamu (Universal Declaration of Human Rights (UDHR)): www.un.org/en/documents/udhr/

c) Wasimamizi wa Azimio La Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa (UN Declaration of Human Rights Defenders): http://www.ohchr.org/EN/Issues/SRHRDefenders/Pages/Declaration.aspx

d) Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu (African Charter on Human and Peoples Rights):http://www.achpr.org/instruments/achpr/, na itifaki zake nyingine

e) Protokali za Shrikisho za Afrika Mashariki (East Africa Community protocols):

http://www.eac.int/legal/index.php?option=com_docman&Itemid=47



f) Mpango wa Hatua ya Umoja wa Mataifa kuhusu Usalama wa Wandishi wa Habari na Uhalifu Usioadhibiwa (UN Plan of Action on the Safety of Journalists and the Issue of Impunity): http://www.unesco.org/new/fileadmin/MULTIMEDIA/HQ/CI/CI/pdf/official_documents/UN_plan_on_Safety_Journalists_EN.pdf

g) Karatasi ya Dondoo No 27: Katibu Maalumu ya kuendeleza na kulinda haki ya uhuru wa maoni na kujieleza (Fact Sheet No 27: Special Rapporteur on the promotion and protection of the right to freedom of opinion and expression): http://www.ohchr.org/EN/ISSUES/FREEDOMOPINION/Pages/OpinionIndex.aspx

h) Viashiria vya Usalama vya wandishi wa Habari: Ngazi ya kitaifa – Kutotokana na Viashiria vya Uendelezaji wa Vyombo vya Habari vya UNESCO (Journalists' Safety Indicators: National Level – Based on the UNESCO's Media Development Indicators): www.unesco.org/

i) Global Compact Network Kenya: www.globalcompact.or.ke/

j) Miongozo ya Kanuni za Uongozi kwa ajili ya Wamiliki na Mameneja wa Vyombo vya Habari wa Afrika, Chapisho la African Media Initiative (Leadership Guiding Principles for African Media Owners and Managers, a publication of the African Media Initiative): www.africanmediainitiative.org

Wakiwa wafanya kazi kwenye Kaunti, wandishi wa habari wanapaswa kutambua sheria maalumu zinazogusa uhuru wa kujieleza ili wasifanye kinyume na kinachoruhusiwa kisheria.

## Wanahabari na usalama wao


Kujiweka hatarini ni uchaguzi wa mtu binafsi. Maamuzi hufanywa kutokana na hisia za kuwajibika, ushujaa wa kibinafsi na wakati mwingine yote mawili. Kumbuka wanahabari waliojeruhiwa au kuuawa wanakuwa sehemu ya hadithi, sehemu ya tatizo, na hawawezi kufanya kazi zao. Wapendwa wao hubaki wakitaabika ikiwa mwanahabari amefariki. Hatimaye hadithi husahaulika hata kama mwanahabari hakusahaulika. Ni muhimu wanahabari kupima usalama wao kwanza kabla hawajaanza kuchunguza hadithi hatarishi. Tumia ujuzi wako na baki hai ili ubadilishe maisha ya wengine ili yawe bora zaidi. .

# MAANDALIZI YA MSINGI: ULINZI NA USALAMA KABLA YA KUANZA KAZI

*"Kwa kushindwa kujipanga, unajipanga kushindwa."*
Benjamin Franklin, mmoja wa waanzilishi wa Marekani.

## Tathmini ya hatari

Ukiwa kama mtendaji katika operesheni, wewe na shirika lako la habari ni lazima kujijengea mazoea ya kutathmini hatari kabla ya kufanya kazi yoyote. Uzoefu wako ndio uwe mwongozo wako kwa sababu matukio ya habari huwa hayatabiriki sana. Usitegemee kwamba muda wote mambo yatatokea kama yalivyopangwa au kama inavyopasa yatokee. Kazi ya kawaida inaweza kubadilika na kuwa kazi inayohatarisha maisha yako. Katika hatua ya mipango,



unapaswa kuwa na uwezo wa kumshirikisha mhariri matatizo yoyote na mtazamo wako wa hali ya hatari inayokukabili. Kimsingi, mchakato wa mipango lazima uzingatie yafuatayo, hususan kama unatarajia kufanya kazi katika mazingira ya vita au kuchunguza uhalifu, ambayo hakika ina viashiria vya hatari:

i) Orodha ya watu muhimu na mawasiliano yao kwa ajili ya dharura, yaani wafanyakazi wenzako, ndugu zako, washirika wa mitaani, polisi, mashirika ya kiraia, Shirika la Msalaba Mwekundu, n.k.

ii) Mpango au mkakati wa mawasiliano wa kuhakikisha kuwa kila wakati unaweza kuiarifu ofisi mahali unapokwenda kufanya kazi

iii) Kutambua hatari zote zinazojulikana katika eneo unalotoa ripoti. Kwa maneno mengine, unapaswa kufanya utafiti wa eneo unaloenda kufanyia kazi, mazingira, hali ya hewa, mila na desturi, mtazamo wa wenyeji kuhusu shirika lako la habari, miundombinu ya mawasiliano, upatikanaji wa huduma za msingi kama vile maji, chakula, malazi, huduma za afya na usalama.

iv) Kuwa na muhtasari wa mpango wa dharura wa kushughulikia hatari zilizotarajiwa

v) Fanya tathmini ya mahala pa kukaa na pa kukimbilia endapo itabidi. Panaweza kuwa kanisani, msikitini, polisi, shule au eneo la ofisi ya Gavana.

vi) Kuwa na mpango wa usafiri ambao ni wa kina na unaoonyesha nafasi ya kusimama kwa ajili ya kutengeneza gari.

vii) Jifunze kutoka kwa wenye uzoefu. Kama wewe ni mgeni katika taaluma ya uandishi wa habari, mada au jukumu fulani waombe wenzako wenye uzoefu wakupe ushauri na kukufundisha kazi. Mada zingine zina hatari kwa mfano uhalifu, vita au ripoti zinazohitaji uchunguzi kuhusiana na usalama, utawala na rushwa. Kama unafuatilia mada fulani, unapaswa kuelewa hatari zinazoweza kutokea kwa kufuatilia hiyo mada. Ni vema kuwatambua wahusika wakuu na kuelewa nia zao, pia kutambua mapungufu yako katika kutoa kuripoti katika hali ya usalama.

viii) Jaribu kwa kadiri unavyoweza kujitegemea.

ix) Hatua utakazochukua ndizo zitakazochangia kufanya mazingira ya kazi yawe salama.

x) Utathmini wa hatari unafaa kuzingatia mambo matatu yafuatayo. Ni kitu gani kinachoweza kuwa tisho kwangu? Kisha orodhesha mambo yanayokusaidia pamoja na udhaifu wako unapofanya kazi. Kwa mfano, mashirika ya umma yanayoweza kukusaidia, kuelewa lugha inayozungumzwa pamoja na desturi ya watu ili uweze kujisaidia. Hatimaye, jiulize udhaifu wangu ni upi? Watu wasioelewa lugha huhitaji wakalimani. Fahamu kuwa, ingawa wakalimani wamependekezwa, hali ya kuwatumia inaweza kuzua utata penye habari ya siri au kuhusu usiri wako mwenyewe. Kufanya utathmini huu wa haraka kutakusaidia kupunguza hatari pamoja na kubadili mipango.

*Tazama kiambatisho I & III kwa maelezo zaidi*

**Hali ya ukame na nusu-ukame katika wilaya za kaskazini na kaskazini-mashariki mwa Kenya zinaleta changamoto hasa kutokana na historia ya migogoro ya kupigania raslimali adimu. Kwa hiyo, tukio lolote la uandishi wa habari kwa mfano katika eneo la Baragoi, linahitaji mipango na maandalizi ya kina kwa sababu ya hali ya Serkiali kutopajali kwa miaka mingi hadi kupelekea kutowepo kwa miundombinu na huduma za msingi. Ukivuka mpaka, eneo la Somalia ni la hatari na kuna wandishi wa habari waliopoteza maisha yao wakiwa wakifanya kazi huko. Maeneo mengine ambayo yanahitaji mipango ya kina ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, na maeneo yanayoshikiliwa na Boko Haram huko Nigeria.**

## Vitu Muhimu

Kutegemeana na eneo la kazi na hali ya usalama, kila mwongozo wa usalama lazima uwe na orodha ya vitu vya muhimu kwa usalama na ulinzi wa wandishi wa habari. Ni muhimu kuvifahamu vitu hivi, ila mwandishi wa habari na mhariri wake wanapaswa kuamua ni vitu gani viwekwe kwenye sanduku lenye vifaa vya kusalimika (yaani, 'survival kit'). Yafuatayo ni ya muhimu kuwepo kwenye sanduku lolote la aina hiyo:

i) Sanduku la huduma ya kwanza lenye dawa za maumivu, bandeji, glovu, vitambaa vya kujifuta (yaani 'wet wipes'), na dawa antiseptiki kama "Dettol" au "Savlon". Kisanduku kiwe pia na bandeji za pumzi, dawa za kuzuia damu kuvuja na visodo ili kusaidia majeraha ya risasi.

ii) Maji na dawa za kusafisha maji machafu. Water and water purification tablets.

iii) Tochi na betri za akiba

iv) Maji ya kunywa

v) Kitambulisho cha wandishi wa habari au barua ya utambulisho kutoka kwa shirika lako ama Braza la Wandishi wa Habari la Kenya.

vi) Sanduku la safibinafsi ("toilet kit") lenye vitu kama mswaki, dawa ya mswaki, chanuo n.k.

vii) Simu ya mkononi yenye betri na simkadi ya akiba ama simu ya mkononi inayotumia nguvu ya sola.

*Katika hali ya hatari sana orodha itakuwa pia na vifaa vya kujikinga kama kifunika pua, miwani ya kujikinga, kofia ya kujikinga na vesti ya kuzuia risasi.*

**Mfuko wenye vifaa muhimu kama vile kadi ya mchangiaji damu, au ukiwa katika eneo lenye vita, kadi ya kundi lako la damu na orodha ya vitu vinavyokudhuru, pesa ya akiba, nakala za kitambulisho cha uraia na picha za paspoti, nakala za mawasiliano muhimu ya wafanyakazi wa vyombo vya habari pamoja na mpango wa tathmini ya hatari au maafa.**

# KUKABILIANA NA HATARI

Mashirika ya habari yanapaswa kutambua wajibu wao wa kuwaunga mkono wandishi wao wa habari, wawe ni wafanyakazi, wandishi wa habari wa kudumu au huria wakiwa katika kazi walizokabidhiwa. Wahariri wanapaswa kuwa wa kweli kuhusu utayari wa mashirika yao kuwaunga mkono. Kutotoa ufafanuzi wa kina kabla ya mwandishi wa habari kuanza kufuatilia habari kunaweza kusababisha matatizo na usumbufu baadaye.

Kuwa na ufahamu kwamba mazingira yanaweza kubadilika. Hakuna tathmini au Protokali ya usalama iliyokuwa kamilifu, lakini muhimu zaidi, ni lazima izingatie mazingira yako ya wakati huo. Hakikisha una taarifa kuhusu mambo yanayoendelea katika mazingira yako na ambayo yanaweza kuathiri usalama wako; fanya tathmini juu ya hali ya usalama wako mara kwa mara. Ikiwa kuna vitisho (kuna uwezekano kuwa mtu atakudhuru au ashushe hadhi yako makusudi au aharibu mali kupitia ghasia). Ni muhimu kutilia maanani mambo yafuatayo:

1. Tambua habari muhimu kuhusu vitisho.
2. Tambua mfululizo wa jinsi mambo yanafanyika, au kama ni tukio la wakati mmoja.
3. Tambua nia ya vitisho.
4. Tambua chanzo cha vitisho
5. Fanya maamuzi yenye mantiki kuhusu kuwepo kwa tisho

Ni muhimu kuelewa kwamba sio vitisho vyote vinahusu kazi yako. Mambo ya kimsingi yatakuwezesha kutofautisha swala hili. Baada ya kutofautisha, ni muhimu kuyaandika, kuyatathmini, na kuyashughulikia.



# JINSI YA KUFUATILIA AU KUKABILIANA NA VITISHO VYA KUUAWA AU KUFADHAISHWA

Katika asilimia kubwa ya kesi zilizoripotiwa, vitisho vinatumwa kwa simu au ujumbe mfupi wa simu kutoka kwa mtu asiyejulikana. Vitisho hivyo vinatumwa mara nyingi ili kumnyamazisha mwandishi wa habari. Wanahabari wengine walipokea kadi za kuwaliwaza, eti mwanahabari mwenza ama jamaa wake amefariki. Ni muhimu kuvichukulia vitisho hivi kwa makini. Utafiti wa CPJ unaonyesha kuwa asilimia 35 ya wandishi wa habari waliouawa katika kipindi cha miaka 20 iliyopita walitumiwa kwanza vitisho. Vituo vya habari havina budi kuwapa wandishi wa habari wanaokabiliwa na vitisho vya mara kwa mara vinasa sauti (au wakati mwingine simu zenye uwezo wa kunasa sauti). Kupatikana kwa rekodi ya vitisho kutasaidia wandishi wa habari kuweza kuripoti hivyo vitisho kwa ajili ya uchunguzi. Njia nyingine ya kuzuia hivyo vitisho ni kwa kumuarifu anayetoa vitisho kwamba anarekodiwa.

Ni muhimu sana kuripoti vitisho kwa wafanyakazi wenzako waaminifu, mhariri wako, Baraza la Habari la Kenya na polisi. Hakikisha unafahamu kwa kina maelezo kamili kuhusu hilo tishio, ikiwemo asili yake, jinsi lilivyotumwa na wakati gani.

Hakikisha vitisho vinatangazwa kwa njia ya vyombo vya habari, mablogu, twita, ‘facebook’ na njia zingine za mawasiliano. Kumbuka pia kuripoti vitisho kwa makundi yanayopigania uhuru wa wandishi wa habari ya ndani na nje ya nchi kwa mfano Kamati



ya Kulinda Wandishi wa Habari (Committee to Protect Journalists, CPJ). CPJ italitangaza hilo tishio au kutunza usiri wake kutegemea na matakwa yako.

Wandishi wa habari wanaofanya kazi katika mazingira hatari wanaweza kufikiria kubadili mada wanayofuatilia kwa muda au kabisa. Wahariri wanapaswa kushauriana na mwandishi wa habari anayetishwa na kuwezesha kubadilishwa kwa kazi aliyopewa ikiwa ameomba hivyo kwa sababu za kiusalama. Baadhi ya wandishi wa habari wamekuta kwamba kwa kuachana na mada nyeti kwa muda kumesaidia kupunguza hali ya uhasama.

## Uchunguzi na Kuchunguza Wanaochunguza

Uchunguzi hufanywa kwa sababu zifuatazo:

- Kujua mambo yanayofanywa, wakati gani, na nani/pamoja na nani.
- Kutumia habari hiyo baadaye ili kushambulia watu au mashirika.
- Kukusanya habari inayohitajika kutekeleza mashambulizi
- Kukusanya habari ili kuchukua hatua za kisheria au hatua zingine za kudhulumu (bila mashambulizi ya moja kwa moja.
- Kukufadhaisha wewe au wafuasi wako, au watu wengine mnaofanya kazi pamoja.

Kumbuka kwamba sababu ya kufanya uchunguzi inaweza ikabadilika kulingana na habari inayopatikana ama wakati hali ya kisiasa inapobadilika. Elewa kuwa uchunguzi sio shambulizi na sio lazima isababishe shambulizi.

Kuchunguza Wanaokuchunguza kunaweza kukakusaidia kujua ikiwa unachunguzwa. Ni muhimu kujua mambo yaliyo karibu nawe, hasa sehemu unazotembelea mara nyingi kama vile nyumbani na afisini. Kuwa makini na watu au magari yanayoonekana kuwa sio ya kawaida. Baadhi ya watu wanaoendesha uchunguzi wanaweza kuwa wakifanya shughuli za kawaida kama vile wahudumu wa boda boda. Hata hivyo, wanapojishughulisha na mambo yako kila wakati, kunaweza maanisha kuwa unachunguzwa. Kuna sababu nyingi za watu kufanya uchunguzi, ikiwa ni pamoja na kupata pesa, watu kushurutishwa kufanya hivyo, wanaweza kuwa washiriki wa washambuliaji, ama mchanganyiko, au hali zote mbili. Mara nyingi, huwa hawataki ujue kuwa wanakuchunguza. Watatumia watu tofauti, magari tofauti, boda boda, n.k.

**Uzuri wa kuchunguza wanaokuchunguza ni kuwa anayekuchunguza hukosa kujua kuwa umetambua anakuchunguza**

Njia nzuri ya kujua ikiwa unachunguzwa, ni kuchunguza watu unaodhania kuwa wanakuchunguza bila ya wao kujua. Unaweza kutumia mtu mwingine unaye mwamini akusaidie kupanga wakati wa kuondoka nyumbani au afisi na utazame anayekufuata au kile anachofanya. Hii inajulikana kama Kuchunguza anaye kuchunguza. Uzuri wa kufanya hivi ni kuwa mtu anaye kuchunguza hukosa kujua kuwa umetambua anakuchunguza. Usikabiliane na anaye kuchunguza kwani hiyo inaweza sababisha vita. Ushauri unawafaa zaidi wale wanaoishi mijini au semi zenye kiji midogo. Hata hivyo, watu wanaoishi mashinani huwa waangalifu wanapowaona watu wasiowajua.

Aidha ikiwa unashughulikia tukio kubwa, unafaa kuelewa vyema mambo yanayoendelea karibu nawe, pamoja na mabailiko ya tabia ya watu. Ikiwa muuzaji wa magazeti ataanza kuuliza walinzi wa usiku mambo kukuhusu, basi unafaa kuwa na shauku.

Sababu ya uchunguzi kufanywa ni kwamba unaweza kukusaidia kuamua hatua ya kuchukua. Ikiwa unachunguzwa, ni vizuri kuepesha mtu mwingine kutokana na hatari. Baada ya kutathmini hatari, unafaa kuweka mipango ya awali, na kujiandaa kwa mambo yasiyotarajiwa. Kwa mfano ikiwa ni habari kuhusu chanzo cha uhabari, basi unaweza tafuta mtu mwingine atakayepeleka habari ile, au unaweza tumia mafumbo ili ikiwa utafumia fumbo fulani kwenye habari, basi ajue kuwa hautafika mahala mlipoagana. Ni muhimu kujua kuwa uchunguzi unaweza fanywa na mtu yeyote – mwanamme au mwanamke. Unafaa kukumbuka mambo yaliyotajwa unaposhughulikia hatari na uandae mkakati mzuri.

## Maandamano na vurugu

Wandishi wa habari wanaofuatilia taarifa kuhusu maandamano na vurugu wamejipata kwenye hatari kutoka pande zote kwa wakati moja. Kwa mujibu wa utafiti wa CPJ, karibia wandishi wa habari 100 wamefariki wakati wakifuatilia taarifa kuhusu maandamano na vurugu za wenyewe kwa wenyewe katika kipindi cha mwaka 1992 hadi mwaka 2011.

### Vidokezo:

- Kuwa na ufahamu juu ya eneo lako wakati wote. Hakikisha hujiweki kati kati ya waandamanaji na polisi.
- Tafuta njia za kutokea kabla ya kuelekea sehemu zenye vurugu.
- Kaa upande wa waandamanaji. Mawe na makombora huwa yanarushwa na watu waliopo katikati ya kundi kama njia ya kuepuka kuonekana kwa kujichanganya miongoni mwa watu kwenye kundi.
- Vaa nguo zinazofaa.
- Hakikisha una kitambulisho cha mwandishi wa habari.

## Maeneo ya ajali, moto na uokoaji

Jukumu la kwanza la yeyote kati ya watu wale wa kwanza kufika katika maeneo ya matukio ya dharura – wakiwemo polisi, wafanyakazi wa gari la wagonjwa, askari wa zimamoto pamoja na wandisihi wa habari – ni kujikinga kwa kukagua hilo eneo na kutanabahi vitu vinavyoweza kuwa vya hatari.

Heshimu mipaka iliyowekwa na mamlaka husika. Mara nyingi, kumfadhili afisa polisi au kutoa taarifa kuhusu mamlaka husika inavyoshughulikia hilo tukio kunaweza kukusaidia kupata nafasi bora zaidi kwa ajili ya kuripoti au kupiga picha. Kuvuka mipaka iliyowekwa na polisi au kutotii amri ya polisi kunaweza kupelekea kuwekwa korokoroni. Wakati wote wandishi wa habari wanaofuatilia habari za dharura au za uokoaji wanapaswa pia kuonyesha wazi vitambulisho vyao.

## Vitu vya kubeba – kukabiliana na vitoa machozi na silaha zingine zinazoweza kukudhuru

- Limau inaweza kupoza majeraha kutokana na kuungua
- Taulo bichi linaweza kukinga uso wako dhidi ya vitoa machozi
- Miwani ya kuogelea inaweza kukinga macho yako dhidi ya vitoa machozi

Kuwa mtulivu pindi unapowekwa korokoroni. Fahamu kwamba endapo utaamua kupinga kuwekwa korokoroni unaweza kujiweka katika matatizo zaidi. Ukiamua kutopinga jitahidi kuwa mweledi unapojieleza kwamba wewe ni mwandishi wa habari unayefuatilia habari za hilo tukio. Lakini, rekodi mfuatano wa tukio zima, majina ya maafisa waliokuweka rumande na mashtaka yako kama yapo.




## Uhalifu Uliopangwa na Rushwa

Kazi ya ufuatiliaji wa taarifa za uhalifu uliopangwa na rushwa ni hatarishi. Mara nyingi ni vigumu kutofautisha kati ya vikundi vya siasa na vikundi vya wanamgambo, hali inayowaongezea hatari wandishi wa habari. Hii ni hasa kwa maeneo kama sehemu za kati ya Kenya, Nairobi, Nyanza na Pwani ambapo vikundi vya jinai kama Mungiki, Sungusungu, Baghdad Boys na makundi ya kigaidi kama vile Taliban na al-Shabaab wanaendesha shughuli zao bila woga wala kujali. Hali hii inapelekea kupungua kwa msaada wowote wa usalama kwa wandishi wa habari.



# MAANDALIZI YA MSINGI



Mbinu ya kuchunguza taarifa za jinai, pamoja na kufuatilia taarifa za uhalifu uliopangwa, inategemea sana mambo ya ndani ya eneo la matukio hayo. Kwa mfano, mbinu itakayotumika kufuatilia taarifa kuhusu shughuli za Sungusungu wa Kisii ni tofauti sana na ile itakayotumika kufuatilia shughuli za al-Shabaab au migogoro ya wezi wa ng'ombe katika maeneo kama vile Baragoi. Wandishi wa habari wanapaswa kujielimisha kuhusu maeneo yenye jinai, njia za kuingilia na kutokea, maeneo yenye usalama yanayofikika kwa urahisi kwa ajili ya kukutana na vyanzo vya habari.

Mhariri angalau mmoja lazima awe na taarifa kuhusiana na kazi inayofanywa na mwandishi wa habari anayefuatilia masuala ya jinai, vyanzo vyake vya habari na maendeleo yake katika kupata hizo taarifa. Wandishi wa habari wa kujitegemea wanapaswa kuwa na wenza walio waaminifu watakaowapa taarifa hizo zote.

Unapomfuata mhusika mwenye uhasama, unapaswa kuambatana au kufuatiliwa na mwanahabari mwenza. Ili kupunguza uwezekano kulengwa kwa kulipiza kisasi, unapaswa kuwaarifu vyanzo vyote vya habari za jinai, hasa wale wenye uhasama, kwamba hufanyi kazi peke yako na kwamba shughuli zako zote zinafuatiliwa kwa karibu na shirika la habari au mwenzako. Tafuta afisa mwandamizi wa kusimamia sheria na ujenge uhusiano wa karibu ili wewe na wenzako muweze kumkimbilia pindi dharura inapotokea.

## Kuandaa mpango wa uchunguzi

Ni muhimu kufanya tathmini ya usalama kabla ya kuanza kazi. Unapofuatilia taarifa kuhusu makundi hatarishi kama vile Mungiki, watuhumiwa wa makosa ya jinai au ugaidi, tathmini hiyo ni lazima iambatane na mpango wa dharura iwapo mwandishi wa habari au vyanzo vyake vya habari vitakuwa hatarini. Tathmini inatakiwa kuwatambua wahusika walio hatari zaidi, pamoja na masuala nyeti zaidi katika uchunguzi ili uweze kutathmini hatari inayoweza kujitokeza. Pawepo na utaratibu bayana juu ya wakati gani na jinsi ya kuwasiliana kwa usalama na wahariri na wanahabari wenzako. Fanya kwanza mahojiano na vyanzo vya habari ambavyo una imani nao zaidi kisha uendelee taratibu na vyanzo ambayo vina hali ya uhasama. Punguza taarifa unayotoa kuhusiana na uchunguzi wako.

## Kuwafuata wahusika wa habari wenye uhasama

Uamuzi wa kuwafuata watuhumiwa wa makosa ya jinai kwa ajili ya kuwahoji, na namna ya kuwatafuta inategemea mambo kadhaa. Ni muhimu kujua wasifu wa maafisa wa utekelezaji wa sheria na kama ni watu amabao unaweza kuwategemea kutatokea matatizo katika uchunguzi unaofanya. Katika uchunguzi wowote wa masuala ya jinai, kumbuka kwamba hatari kubwa inaweza isiwe kuripoti kuhusu makundi ya uhalifu, bali kwenye mtandao wa rushwa unaowalinda.

### Vidokezo:

- Andaa habari ya kuaminika itayakofunika ukweli wa uchunguzi wako.
- Kile kipindi cha muda mfupi kabla habari kurushwa hewani mara nyingi ndicho cha hatari zaidi. Wandishi wa habari wanapaswa kuwa makini na watu wanaoongea nao na kutojionesha.
- Katika mipango ya kufanya mahojiano na mhusika mwenye uhasama, vyumba vya habari na wanahabari wenzako lazima wafahamishwe.
- Kuwa na mwanahabari mwenzako au mtu mwingine anayekufuatilia.



## Kupata habari

Katiba ya Kenya inatambua haki ya kupata habari. Kanzi (databenki) ya taarifa kwa umma, iliyozinduliwa mwaka 2011, inapatikana. Hata hivyo, upatikanaji wa nyaraka za serikali kwa njia rasmi mara nyingi ni vigumu, ingawa ni suala muhimu katika taarifa za uchunguzi. Kuwa na uzoefu wa kutumia nyaraka za serikali kama dondoo, mbali na kuwa na manufaa sana, pia inaweza kupunguza utegemezi wa habari kutoka kwa vyanzo vilivyo na uhasama.

Ikibidi wandishi wa habari kutumia njia zisizo rasmi kupata takwimu za serikali, ni lazima kuchukua tahadhari ili kuepuka kumfichua aliyetoa (chanzo) nyaraka nyeti. Kufanya mahojiano kadhaa kama njia ya kufunika ukweli wa chanzo cha taarifa kunaweza kusaidia kulinda chanzo cha hizo nyaraka. Matumizi ya nyaraka pia yanaweza kuhamisha ujasiri kutoka kwa chanzo cha habari kwenda kwa mwandishi wa habari. (Tazama sehemu ya mawasiliano na habari kwenye wa mwongozo huu).

## Jitihada za pamoja

Wandishi wa habari wanagundua njia mbadala ya kuchapisha taarifa zinazoweza kuwaweka hatarini. Mtumizi ya majina bandia au kuripoti chanzo cha taarifa kama "mwandishi mfanyakazi" ni hatua zinazotumika mara kwa mara kuwalinda wandishi wa habari.

Mashirika ya habari yanaweza pia kushirikiana kutoa taarifa kuhusu mada ambazo ni hatarishi kwa wandishi wa habari, kwa kubadilishana taarifa na kuchapisha habari wakati sambamaba bila shirika lolote kudai umiliki wa hiyo habari. Njia hii imethibitika kuonyesha mafanikio katika kupunguza hatari dhidi ya mwandishi wa habari na kuwezesha kufuatilia mada zilizohatarishi. Huko Burundi, wanahabari wanatumia mfumo uitwao "synergie", yaani ushirikiano, vyombo vyote vya habari vinachapisha / kurusha hewani habari nyeti sambamba ili kuepuka kulengwa kwa chombo kimoja cha habari. Huku Kenya njia hii inaitwa kujasiri kwa pamoja au kutawanya hatari. Kushirikiana nje ya mipaka ya nchi ni njia nyingine ya kupunguza hatari.

Katika jitihada za kupunguza tishio la vikwazo kutoka kwa Serikali wakati wa chama kimoja cha utawala cha Kenya African National Union (KANU), wahariri mara kwa mara walishirikiana kutoa taarifa nyeti. Ilikuwa ni njama, kwa kweli, ambapo mhariri mmoja aliachia haki yake ya kumiliki taarifa na kukubali kushirikiana na vyombo vya habari ambavyo ni wapinzani ili wajasiri pamoja. Katika mazingira yaliokithiri zaidi, kulikuwa na mpango wa makusudi wa taarifa nyeti kutolewa na gazeti la nje ya nchi. Sambamba " mpanga njama" aliyeko Nairobi anaendeleza hiyo taarifa kabla vyombo vingine vya habari, kisha anaendelea kutafuta fursa nyingine ya kukabiliana na huo mfumo wenye vikwazo. Kwa njia hiyo, mhariri jijini Nairobi anaweza kujitetea kuwa alikuwa anachapisha hadithi ambayo tayari ilichapishwa mahali pengine.

## Maeneo yenye uhalifu na ugaidi

Inaweza kuwa vigumu kufuatilia taarifa kwenye maeneo yenye uhalifu na ugaidi. Ni muhumu sana kuangazia ulinzi wako binafsi. Wakati wa vurugu kama mashambulizi ya kigaidi kama vile katika maduka ya Westgate Septemba 21, 2013 jijini Nairobi, kuwa makini kutojiingiza kwenye misukosuko. Swali la kujiuliza ni kama wahusika bado wanaweza kuwa wanazunguka katika hilo eneo. Katika kesi ya mashambulizi ya kigaidi au hatua nyingine iliyoundwa kwa madhumuni ya kuvutia umma, chukulia kwamba yanaweza kufuatiwa na mashambulizi mengine ya nyongeza.

Kadri inavyowezekana vitambulisho vyako vionekane wazi unapokuwa kwenye maeneo yenye uhalifu. Epuka kukwaruzana na mamlaka husika, bali ni muhimu kuwa na uhusiano mzuri na viongozi waandamizi wa usimamizi wa sheria.

Mashahidi na waathirika wengine wa matukio ya vurugu wanaweza kuwa wamechanganyikiwa au kupatwa na mshtuko. Hivyo, heshimu matakwa ya waathirika hao kuhusu kuhojiwa au hisia zao kurekodiwa. Kuonyesha heshima kwa namna hiyo, kutapelekea kupata ushirikiano wa waathirika hao na kuwezesha wandishi wa habari kupata habari zaidi. Polisi na waokoaji pia wanaweza kuwa wamepatwa na mshtuko. Elewa kwamba huu muda unaweza kuwa sio muafaka kuwahoji waathirika au mamlaka husika.

## Usafiri na vifaa vya uandishi wa habari

Magari ya wandishi wa habari lazima yawe na vifaa vya dharura, ikiwa ni pamoja na chombo chenye vifaa vya huduma ya kwanza, miwako ya barabarani na mablanketi. Mameneja wanapaswa kutafiti mahala pa kukodisha magari ya dharura, vifaa vya mawasiliano na vifaa vingine muhimu. Mambo yote haya pamoja na maelezo ya mawasiliano yanapaswa kuorodheshwa katika mpango wa dharura. Mameneja wanapaswa pia kujua jinsi ya kupata mafuta ya akiba wakati wa dharura. Wafanyakazi walioko kwenye operesheni wanapaswa kuzingatia usafiri wa uhakika na ulio salama katika mipango ya kazi.

Magari hulengwa mara nyingi ghasia zinapotokea. Ikiwa uko kwenye gari inayofyatuliwa risasi, unafaa kutathmini hali


**Gari linaweza likalengwa kwa urahisi. Hukuweka kwenye hatari ya kujeruhiwa na vioo au milipuko ya mafuta ya gari, pamoja na moto.**

ilivyo, inagawa ni vigumu kufanya maamuzi mahsusi. Kwa ujumla, ni vyema kuchukulia kuwa gari linaweza kulengwa kwa mashambulizi, hivyo basi kitu cha busara ni kushuka mara moja na kujificha. Gari linaweza likalengwa kwa urahisi. Hukuweka kwenye hatari ya kujeruhiwa na vioo au milipuko ya mafuta ya gari, pamoja na moto. Ikiwa moto hauko karibu sana, jaribu kuendelea na safari hadi ufike mahala pa kujificha.

## Kukamatwa au kuwekwa kizuizini

Kama ukikamatwa au kuweka kizuizini, kumbuka kuwa mtulivu na mweledi. Usijiingize kwenye malumbano yanayohusu haki zako. Kama unaweza kuwa na hoja ya msingi kujadiliwa, hicho ni kitu sahihi lakini ikiwa afisa hajavutiwa nayo kwa mtazamo wako, ni bora uachane nayo.

Ukiambiwa hupo huru kuondoka au umewekwa kizuizini, inasisitizwa sana kuwa ufanye haraka kile unachoambiwa, lakini wasiliana na wenzako au uongozi kuhusiana na hilo suala ili kulifanyia kazi. Afisa polisi au mamlaka ya serikali yoyote haihitaji kitu kikubwa zaidi ya wewe kuafiki wanachokuambia. Unapogoma, kitendo hiki kinawafanya waongeze nguvu ambayo wanahisi inahitajika kutosheleza mpango wa kukuweka chini ya ulinzi.



Ni muhimu kujitambulisha mwenyewe kama mwandishi wa habari mara nyingi iwezekanavyo, ili kusiwe na maswali ya wewe ni nani au lengo la kuwa pale ni lipi. Ni muhimu kukumbuka kuwa chochote unachosema kinaweza kutumika dhidi yako na kusababisha tuhuma za ziada.

Kitu cha kwanza mahususi unapoanza, muombe afisa mtoa ruhusa, (mfano: OCPD, DCIO, au OCS), apate taarifa kuwa mwandishi wa habari ametiwa kizuizini au amekamatwa. Kama inawezekana, taarifa za kukamatwa zipelekwa kwa mhariri wako. Na ikiwezekana mjulishe mwanasheria. Kama upo nje ya nchi, wasiliana na ubalozi wa nchi yako.

Kama umekamatwa katika maeneo ambayo vyombo vya habari havifiki, sisitiza kuhamishiwa kwenye kituo kinachofahamika na kina utambulisho maalumu. Sehemu ambazo hazitambuliki zinaweza kuwa kituo cha askari wa doria, kituo cha polisi na utawala wa polisi.

**Afisa polisi anaweza kuhitaji kuona taarifa zako kama picha, rekodi au nyaraka/mafaili. Kumbuka kuwa huhitaji kutoa idhini juu ya ombi kama hilo. Pia wanaweza kujaribu kukutisha, kukushurutisha au kukuogopesha uwape ruhusa, lakini inabidi utoe ruhusa kwa ridhaa yako. Hata kama askari akizichukua kamera au vifaa vingine vya kazi hana haki ya kuangalia mpaka apate ruhusa.**



Kumekuwa na matukio ambayo polisi wamekuwa wakiwaamuru wandishi kufuta nyaraka au wamekuwa wao wenyewe wakizifuta nyaraka/faili hizo. Tendo lolote ambalo lipo kinyume na sheria alilofanyiwa mwandishi wa habari inabidi liwekwe kwenye kumbukumbu, yaandaliwe na yakabidhiwe mamlaka husika.

## Utekaji nyara na unyang'anyi wa magari

### *Hali ya mateka*

Njia nzuri ya kujikinga na hili ni kuchukua tahadhari, kusafiri kwa makundi kwenye sehemu hatarishi, kuhakikisha kuwa wenzako unaowaamini wanatambua mipango yako na kubadilishana mawazo. Siku za hapo nyuma, woga ulisheheni na hii iliashiria hali ya dharura.

Ukiwa umechukuliwa kama mateka, anzisha uhusiano na watekaji na ikibidi uwatambue viongozi wao, hii hatua itafanya walinzi wao wasiweze kukudhuru kirahisi. Shirikiana na walinzi lakini usijaribu kuwatuliza. Kadiri uwezavyo, waeleze kazi yako kama mwandishi wa habari na kwamba kazi yako hutoa taarifa pande zote inapohitajika.

## Vitisho vya polisi

Polisi wa Kenya wana rekodi mbaya ya namna wanavyowalinda wandishi. Kufuatiwa na matukio ya vitisho kwa vyombo vya habari. Mbayazaidi, wengine wanarubumiwa na watu wenye ushawishi mkubwa, na wengine

wanakodiwa kuvitishia vyombo vya habari, hata pale ambapo kazi za wandishi zinapoonesha kupongeza kazi za polisi. Mwezi mei mwaka huu, mwandishi wa Star, Lydia Ngoolo aliripoti shughuli za kutiliwa shaka nyumba katika mji wa Mwingi, jimbo la kati, akiamini watuhumiwa wa ugaidi wanatumia nyumba hizo kama kituo cha operesheni zao. Badala ya kushirikiana na Lydia, polisi wameripotiwa hivi karibuni, kuanza kutoa vitisho na kueleekeza maswali kwake juu ya upelelezi wake wa kituo cha magaidi. Mara nyingi wandishi wa habari wanaona hawana msaada pale wanapopata vitisho toka kwa maafisa wao, bila kutambua kuwa kuna hatua ambazo taasisi inaweza chukua dhidi ya polisi.

Namna ya kuripoti mwenendo mbaya wa polisi:

1. Peleka malalamiko kwenye idara ya polisi ya karibu.
2. Ukihisi kwamba haupati msaada ukipeleka malalamiko kwenye idara ya polisi iliyokaribu, au utapata madhara zaidi, vitengo vya juu unavyoweza kutoa taarifa ni pamoja na:-
   - Kituo cha polisi kingine ambacho unajisikia vizuri zaidi, Peleka ripoti kwenye kitengo cha mambo ya ndani.
   - Mamlaka Huru ya Usimamizi wa Polisi(IPOA)- popote ukiwapa malalamiko yako, IPOA watafuatilia.
   - Tume ya Maadili na Kupambana na Rushwa.
   - Tume ya Utawala na Haki.
   - Tume ya Taifa ya Usawa na Jinsia.

Kumbuka ni kosa kisheria pale ambapo afisa wa polisi anapoacha kuandika malalamiko yako.



Je, ni taarifa zipi nahitaji kutoa wakati napeleka malalamiko?

1. Jina lako na taarifa za mawasiliano
2. Kilichotokea, ikiwemo tarehe, muda na mahali.
3. Jina na cheo cha polisi aliyehusika.
4. Majina ya watu waliohusika au watu wanaoweza kusaidia katika upelelezi.
5. Maelezo yoyote ya nyaraka au taarifa ambazo zinaweza kusaidia katika upelelezi.
6. Ungependa chombo husika kiyafanyie nini malalamiko yako.

Shirika/jumuiya pia itakua na fomu maalumu ya malalamiko.

### *Ninaweza kuandaa malalamiko bila utambulisho wangu kufahamika?*

Unaweza kuandaa malalamiko bila kuweka majina. Ukiwa na IPOA, unaweza kuwambia wewe ni nani, lakini ukawaomba taarifa zako za utambulisho ziwe siri. Ombi la upatikanaji wa huduma ya ulinzi kwa shahidi kama una wasiwasi juu ya usalama wake toka kwenye taasisi unayoilalamikia.

Kuwasilisha malalamiko kwa:-

**Kituo cha polisi cha karibu**

Unaweza peleka malalamiko yako kwenye kituo chochote cha polisi, na kwa afisa wa polisi yeyote, sio lazima kupeleka malalamiko kwenye kituo cha polisi ambacho polisi aliyekukosea anafanyia kazi. Polisi atarekodi malalamiko na kutoa taarifa kwa IPOA na kitengo cha mambo ya ndani kinachohusu huduma ya polisi. Hakikisha kuwa ombi la malalamishi litapelekwa baada ya hizi ofisi kupitia malalamiko, hii itaonyesha ofisi ya polisi kuwa upo makini na unaweza kufuatilia pale kama polisi husika hafuatilii malalamiko ipasavyo. Kama kuna ukiukaji mkubwa, IPOA itapeleleza. Aidha kitengo cha mambo ya ndani kitafanya upelelezi kisha kama kuna umuhimu, itatoa mapendekezo na hatua zitachukuliwa dhidi ya afisa wa polisi. Kama ni makosa ya kinidhamu, hii itajumuisha:

- Karipio.
- Kusimamishwa kazi kwa muda.
- Agizo la kurudisha pesa.
- Kusimamisha nyongeza ya mshahara.
- Kumshusha cheo.
- Kufutwa kazi.

IPOA itafuatilia iwapo kitengo cha mambo ya ndani kinafanya upelelezi kwa haki na kwa njia ifaayo. IPOA inaweza pia kufanya uchunguzi iwapo itahitajika.

**Tume ya taifa ya huduma za polisi**

Unaweza pia kupeleka malalamiko yako kwenye Tume ya Taifa ya Huduma za Polisi, hata hivyo kwa kawaida huwa hawafanyi upelelezi wa malalamishi mwanzoni, na wanaweza peleka malalamishi kwa IPOA. Tume husimamia ajira, mafunzo na huandaa vikao vya kujadili nidhamu.



**Mamlaka Huru ya Usimamizi wa Polisi(IPOA)**

IPOA ni chombo ambacho kinafanya kazi nje kabisa na huduma za polisi. IPOA:-

- Hupeleleza malalamiko ya utovu wa nidhamu wa polisi ikiwemo majeraha wanayosababisha katika kipindi cha kukamatwa kwa watu au matokeo ya vitendo vya polisi na kupendekeza hatua sahihi.
- Kufuatilia na kupitia mifumo ya polisi na mienendo mibaya.
- Kila baada ya miezi sita, huchapisha matokeo na majibu ya uchunguzi. Hii ni taarifa kwa ajili ya umma.

Baada ya malalamiko kupelekwa, IPOA huanza uchunguzi na ina mamlaka ya kulazimisha watu kuhudhuria mashauri au mikutano pale ambapo watashindwa kutii wito. Baada ya upelelezi, IPOA inaweza kupendekeza yafuatayo:-

- Mkurugenzi wa mashtaka ya umma, hupeleka mashtaka kwenye idara ya makosa ya jinai na humshtaki mhusika mahakamani.
- Polisi watekeleze hatua za kinidhamu zinazochukuliwa dhidi ya maafisa husika.
- Malipo ya fidia.
- Mabadiliko ya taratibu za kipolisi, sera na kusimamia amri zinazotolewa ili polisi wapate mwitikio mzuri katika siku zijazo.

Mkuu wa idara ya polisi atekeleze mapendekezo yaliyotolewa na IPOA kisheria. IPOA ina uwezo wa kuiomba mahakama kulazimisha mapendekezo iliyofanya yafuatwe.

**Tume nyingine**

Ingawa tume nyingine zina madaraka kidogo ya kuchunguza polisi tofauti na IPOA, kupeleka malalamiko kwao inaweza kusaidia kupata uchunguzi halisi wa kipolisi. Ikiwa ni mambo ya rushwa, unaweza kupeleka malalamiko yako moja kwa moja kwenye Tume ya Maadili na Kupambana na Rushwa. Kama ni mambo ya kunyanyaswa kijinsia, unaweza peleka malalamiko kwenye tume ya Taifa ya Usawa na Jinsia.

**Tume ya Taifa ya Usawa na Jinsia**

Kituo cha uadilifu, makutano ya barabara ya Milimani, Nairobi

(au)

Mahakama ya Apollo, mtaa wa Moi, Mombasa.

Barua pepe: report@integrity.go.ke

Simu:020-271-468(Nairobi)/041-231-9081(Mombasa).

**IPOA huchapisha matokeo na majibu ya uchunguzi kuhusu mwenendo mbaya wa polisi**

# MGOGORO UNAOHUSISHA GHASIA YENYE VITA

Mafunzo ya kiusalama yanashauriwa sana kwa yeyote anaekwenda kufanya kazi maeneo hatarishi kama vile sehemu zenye migogoro. Mashirika mengi yakiwemo Baraza la Habari la Kenya, usalama wa kimataifa pamoja na IREX zinatoa mafunzo ya kiusalama kwa wandishi wa habari wa Kenya. Wandishi wa habari inawabidi watambue vyanzo vya migogoro, wahusika na silaha zinazotumika kwa lengo la kujiandaa ipasavyo. Pia inabidi wazitambue tume zingine zinazotoa huduma na msaada kwa wandishi wa habari wanapopata matatizo kama yafuatayo:

- Kwa wanahabari wa kike wanaofanya kazi sehemu zenye vita: http://www.ifj/org/fileadmin/images/Gender/Gender documents/Safety Guidelines for Women working in War Zones EN.pdf
- Tazama kanuni 8 za wanahabari wanaofanya kazi katika sehemu hatari na yenye vita: http://www.rsf.org/IMG/pdf/guide gb.pdf
- Uandishi wa habari unaoleta mabadiliko: kitabu cha wanahabari walioko sehemu zenye ghasia: http://iw3.iwpr.net/sites/default/files/iwpr training manual English.pdf
- Taasisi ya Uandishi wa Habari kuhusu Vita na Amani: http://iwpr.net/build-journalism/modules-and-exercises-journalsim-training
- Kufanya habari kuwa swala la mtu binafsi: kuripoti swala la haki za binadamu, elimu, afya na mambo mengine ya jamii: http://www.icfj.org/sites/default/files/Social Issues.pdf
- Uandishi wa habari, vyombo vya habari na changamoto za kuripoti haki za binadamu: http://www.ichrp.org/files/reports/14/106 report en.pdf
- Kupata amani: Kuripoti Migogoro na Makabila Tafauti: http://asiapacific.ifj.org/assets/docs/056/247/4446738-52feef7.pdf

## Kuungana au kutokuungana na wapiganaji

Kuchagua kuchukua taarifa inayohusisha matumizi ya silaha, au kubaki huru ni maamuzi muhimu. Utafiti wa kina wa hali ya kisiasa, historia na tabia kwa vikundi vyote vyenye silaha na vilivyopo kwenye mgogoro sasa. Kuchagua kujihusisha na upande mmoja wa mgogoro au kubaki huru ni suala la msingi. Kwa mfano Somalia, wandishi wa habari walipongezwa kwa kujiunga na jeshi la ulinzi la Kenya kuhakikisha usalama upo hasa kwenye mazingira yanayobadilika kila wakati, ambapo kuna utekaji na mauaji kwa wandishi wa kigeni mara kwa mara.

Kusafiri na wanajeshi utapata nafasi ya kipekee ya kuwa mstari wa mbele katika kupata taarifa, lakini inakua shida kuelewa mitazamo mingine, ikiwemo kuona matokeo ya mapambano kwa raia. Wandishi wa habari wanaosafiri wenyewe bila jeshi wanakuwa na mtazamo mpana. Vifo hutokea zaidi pia mara kwa mara miongoni mwa wandishi wa habari ambao wanaripoti taarifa za upande mmoja, lakini hatari ya kuingizwa kwenye majeshi inabidi isipuuzwe.

Kama ukiwa kwenye majeshi, kumbuka usiwe tofauti kiasi cha kuonyesha wewe si miongoni mwao. Wapiga risasi hodari wamefundishwa kulenga mpaka vivuli vya maafisa watuhumiwa wa jeshi pinzani. Wandishi wa habari mara nyingine wanahitaji kuvaa mavazi ambayo ni sare ya wapiganaji waliojiunga nao. Kwa kufanya hivo haiwezi kuharibu majukumu yako ya kiutaalamu, lakini unahitaji kuvaa au kubeba vitambulisho vya kukutambua kama mwandishi wa habari.

## Mwandishi wa habari mwenye sare inabidi atarajie kuchukuliwa sawa na adui wa wapiganaji na jeshi pinzani; hiyo ni pamoja na kitendo cha kutokuwepo kwenye kambi ya jeshi.

Wandishi wa habari wanaofanya kazi pekee yao, pia wanatakiwa kutambua muonekano na mwenendo wao kiujumla. Wapiga picha wanaobeba kamera au vifaa vingine wanaweza kuonekana kama wapiganaji. Ukiwa unafanya kazi peke yako, chagua nguo ambazo hazifanani na vifaa vya kijeshi na hazionekani kwa mbali.

Kuandika habari za migogoro yenye vita, uwe na ufahamu wa madhara halisi na ripoti kiujumla. Kitu ambacho kinalazimisha, ripoti halisi toka kwa watazamaji mbali na eneo la vita, inaweza kutazamwa kama si habari ya maana kwa adui. Hii pia ni nzuri kufanyika kweye maeneo yenye itikadi za kisiasa.

*Mambo muhimu ya kujifunza kutoka kwa mtu aliyeungana*


*John Guracha ambaye ni mwanahabari wa shirika la Nation Media Group, alikuwa miongoni mwa wanahabari wa kwanza walioungana na wanajeshi wa Kenya Defense Forces waliokuwa vitani nchini Somalia. Na sasa hujiona kuwa mmoja wa wanahabari waliobobea katika uandishi wa habari sehemu zenye vita. Uzoefu wake unaweza tumiwa kuhakiki Usalama wa Wanahabari. Hivi ndivyo alihusika. 'Niliitwa na wahariri wangu walioniambia wanataka kunituma nchini Somalia nikiwa nimeungana na wanajeshi wa KDF, ili ni ripoti matukio katika oparesheni ya Linda Nchi.'Wanahabari wenzake walikuwa wameambiwa hivyo lakini wakakataa kwa sababu ya usalama wao. Ingawa Nguracha piaalihofia usalama wake, alikubali kwa sababu alitaka kwenda kujionea mazingira mapya. Siku iliyofuata, alifululiza hadi makao makuu ya jeshi jijini Nairobi ambako yeye pamoja na wanahabari wengine walipata mafunzo ya siku tano kuhusu sheria na masharti yanayofaa kufuatwa na wanahabari wanaoandamana na wanajeshi kwenye oparesheni. Ujumbe muhimu ulikuwa, "usiwe mtu anayependa kutembea tembea mahala pageni, na utakuwa salama". Waligundua wako katika hali ngumu walipofika Somalia, kwani walijipata wakilala kwenye mitaro yenye upana wa futi 4 kwa futi 6; wasiwasi; muda kidogo wa usingizi; milio ya kushtusha ya bunduki na milipuko; vifaa vichache vya kutumia na mavazi kidogo ya kujilinda. Anasema, "ninapowaza kuhusu mambo haya, naona wahariri wangu walitaka tu kupata habari, mbali na kuniandaa vilivyo kuhusu kwa kujali usalama wangu."*

Makundi ya watu yanaweza badilika kirahisi kwa taarifa yako, endapo wamegundua "uadui" juu ya taarifa uliyochukua.

## Vituo vya ukaguzi

Kushirikiana na vikundi vyenye silaha kwenye vituo vya ukaguzi ni hatari na huwa haitabiriki. Kabla hujasafiri kwa barabara ndani ya nchi, shauriana na wenzako, maafisa wa jeshi na watu wa kuaminiwa katika eneo lenu na kuamua maeneo yanayoonekana kuwa na vituo vya ukaguzi na waendeshaji wake. Jifunze kabla hatua zote za ukaguzi, kama vile alama za onyo zinazotumiwa na jeshi, utaratibu unaotarajiwa kufuatwa unapokaribia vyombo vya usafiri.

**Kushirikiana na vikundi vyenye silaha kwenye vituo vya ukaguzi ni hatari na huwa haitabiriki**



Katika kilele cha machafuko, baada ya uchaguzi 2008, makundi ya wahalifu yaliweka vizuizi na vituo vya ukaguzi barabarani kinyume cha sheria kuchunguza mienendo ya kuingia au kutoka katika maeneo fulani yaliyodhaniwa kudhibitiwa na chama kimoja au kingine cha siasa. Wengi wa wasafiri waliokua hawajachukua tahadhari pamoja na wandishi wa habari walinaswa katika machafuko ya kabila katika vituo hivyo vya ukaguzi.

*Mambo muhimu ya kujifunza*

*Kwa wakati mmoja, kambi yake ilishambuliwa, na wakaamrishwa na majeshi walale chini hadi adui alifukuzwe.*

*Alijifunza nini?*

- *Vyombo vya habari vinapaswa kuwa na sera kuripoti vita, na inayotoa mafunzo kuhusu mtu binafsi na hisia.*
- *Wanahabari wanapaswa kupewa fursa ya kujiondoa kutoka kwa kazi ile wakitaka.*
- *Lazima wasimamizi wa kazi waweke bima ya maisha kwa wanahabari walioko sehemu hizo.*
- *Sharti wanahabari wapewe mavazi ya kujilinda na wawe na fursa ya kufafanua kuhusu muundo wa mavazi.*
- *Ni muhimu kutoa ushauri nasaha baada ya kazi. Mmoja wa wanahabari wenzake alishtuka sana, kiasi kwamba alijiondoa kutoka kazi ya uandishi wa habari waliporudi nyumbani.*
- *Maelezo kabla ya kazi ni muhimu ili kuongeza maarifa waliyopata kwenye mafunzo.*
- *Ipo haja ya kushauri familia. Mmoja wa walioandama na majeshi alirudishwa nyumbani baada ya mamake kumuona kwenye runinga akiripoti kutoka Somalia huku akidhani alikuwa Mombasa, na hapo akaamuru arudishwe.*
- *Motisha. Baadhi ya walioandamana na wanajeshi walipewa marupurupu kila siku ili kuwapa motisha.*

# HATUA MAALUM KWA MWANDISHI WA HABARI MWANAMKE

Wandishi wa habari wanawake wapo kwenye mazingira hatari sio tu kwasababu ya kazi ila pia kwa jinsia yao. Na hupelekea vitisho na mashambulizi yanyolenga jinsia fulani. Kwa mazingira mengine wanawake wanaingia kwenye hatari zaidi kutokana na kazi wanazofanya, hivyo usalama na ulinzi wao unahitaji msisitizo maalumu. Mtu wa usalama inabidi awalenge wanawake na hatua zinazochukuliwa ziwe maalumu kwa jinsia fulani.

## Unyanyasaji wa kijinsia

Unyanyasaji wa kijinsia au vitisho vimeripotiwa na wandishi wa habari wakati wa kazi. Ripoti ya CPJ ya mwaka 2011, iliwahoji zaidi ya makundi manne tofauti ya wandishi wa habari walioathirika kwenye kazi zilizopita. Wengi wao walioathiriwa



walikua wanawake, ingawa baadhi walikua wanaume. Kinachoendelea ndani ya Tahir square jijini Cairo ni kwamba, wandishi wa habari wanawake wanaoandika habari za matukio kwenye makundi makubwa ya watu, wanakuwa rahisi na walengwa wakubwa wa kunyanyaswa na kushambuliwa, kwa kufuata maelekezo.

Vidokezo;

- Vaa nguo kulingana na mazingira.
- Vaa nguo kulingana na utamaduni wa mahali( mfano; kuvaa hijabu kwa mwanamke kwenye jamii ya kiislamu).
- Wandishi wa habari wanawake wanaweza kuvaa pete za uchumba/ ndoa bila kujali hali zao za ndoa.
- Kujipulizia manukato kunaweza kuzuia watu wabaya.
- Fanya kazi na kundi la wenzako unaowaamini.

**Unapokuwa unaendeshwa kwenye boda boda, epuka kumshikilia mwendeshaji kwa msaada na muonye pale anapokuzoea sana. Weka mzigo wako kwenye nafasi iliyopo katikati yenu mpaka mwisho wa safari. Epuka boda boda pale unapokuwa umevaa sketi fupi.**

Wandishi wa habari wanawake wanatakiwa kutambua kwamba ishara za kuzoeana, kama vile kukumbatiana au kutabasamu hata kwa wenzako inaweza kueleweka vibaya na kuleta uangalifu usiohitajika.

## Yafaa wandishi wa habari wanawake wavae nguo kulingana na mazingira

Usichanganyike kwenye vikundi ambavyo kuna wanaume wengi, wataalamu wanasema; kaa karibu na mwisho na uwe umeshafikiria njia ya kutokea akilini. Taasisi ya kimataifa ya usalama wa habari inapendekeza wandishi wa habari kuwa na taarifa inayoficha ( kwa mfano; "namsubri mwenzangu afike") kama wanapata wasiwasi na uangalifu usiohitajika kwa wengine.

Kama mwandishi wa habari akihisi udhalalishaji wa kijinsia unakaribia kutokea, wataalamu wanapendekeza mwandishi husika aongee kitu chochote ili kubadili sintofahamu iliyopo. Kupiga mayowe au kelele kwa sauti kubwa kwa kuomba msaada ukigundua watu wapo karibu na wanaweza kukusikia ni moja ya vitu vya kufanya. Kutoa maneno yasiyotarajiwa ni njia nyingine, mfano " hivi hiyo ni gari ya polisi?", kuangusha, kuvunja au kutupa kitu kinachomstaajabisha mtu aliyekukamata ni njia ya tatu.

Maelezo zaidi kuhusu ghasia yenye vita:

http://www.ifj.org/fileadmin/images/Gender/Gender documents/Safety Guidelines for Women working in War Zones EN.pdf

# USALAMA WA MAWASILIANO NA HABARI

Kile unachowasiliana na  namna unavyowasiliana kama ni kwa mdomo, kwa maandishi au kwa dijitali ni hali zinazoweza kuingilia usalama wako. Fauka ya hayo, mtizamo na upendeleo wa vyombo vya habari unavyowakilisha, unaweza kuhatarisha na usalama wako, kulingana na habari utakayokuwa unawasilisha kwenye chumba cha habari.

Kama ni habari maarufu inayoshirikishwa kwa wandishi wa habari kwenye vipindi vya mafunzo ya usalama, vinavyorushwa na Baraza la Habari Kenya, inakua kama maigizo, hii hupelekea aina hiyo kukaribisha mtafaruku. Kwa msisimko mwandishi wa habari anamwita mhariri wake kipindi cha mwisho kabisa kunapokuwa na mkutano mzito wa hadhara na kwa sauti kubwa inampa hatua kwa hatua mustakabali wa tukio zima. Bila kupenda anakwenda eneo la mkutano, ambapo watu wamekusanyika, anaelezea jinsi wabunge wa eneo hilo walivyokuwa kimya na makini nje ya mkutano wa hadhara. Kitu ambacho hakugundua ni kwamba watu waliokuwa wamemzunguka walikuwa wanamuunga mkono mbunge. Mwandishi kwa haraka anajifunza ujinga wa kusisimka kwake mara baada ya kupigwa makofi na mateke.

Usalama wa kidijitali una maana ya kulinda mifumo yako ya mawasiliano, ikiwemo vyanzo vya habari dhidi ya wabaya wako. Serikali za kanda zingine kote duniani, ikiwemo Afrika Mashariki, huendeleza matumizi ya teknolojia ya habari na ya kunasa mawasiliano ya mtandao na simu za mkononi. Kuingilia mawasiliano ya simu, barua pepe na ujumbe mfupi kunazidi kuwa  jambo la kawaida kwa watumiaji mbalimbali. Kama umebeba simu ya mkononi au umeunganisha kompyuta kwenye mtandao wa intaneti, kupiga simu au kuangalia barua pepe kunaweza kuonesha taarifa ya pale ulipo, hivyo kumruhusu mtu aweze kufuatilia mienendo yako.

Vidokezo:

- Kumbuka kuhifadhi taarifa zako za siri katika kifaa cha nje ya kompyuta.
- Funga kwa 'maneno ya siri - encrypt' habari iliyohifadhiwa na inayotumwa (k.m. barua pepe).
- Hakikisha kompyuta yako imezimwa unapoondoka kwenye eneo lako la kazi. Hata kwenye chumba cha habari, jihadhari na watu ambao wana kutazama sana, pale ambapo unapofungua barua pepe au kusoma ujumbe mfupi.



- Usitumie kompyuta ya umma kwenye vituo au hoteli kwa mazungumzo ya siri au nyeti. Ikiwa ni lazima utumie, basi pata kutoka kwa mtandao CCleaner na uweke kwenye flashidiski kwa matumizi. Fungua http://securityinabox.org/en/ccleaner_main
- Kila wakati kwenye kompyuta yako au simu unganisha na nywila ('password') ambayo itahitajika wakati wa kuanza kutumia. Nywila zinafaa kuwa ngumu kutambulika. Ni bora kuchanganya herufi kubwa na ndogo.
- Tumia mafumbo mliokubaliana hapo awali, mnapowasiliana mambo nyeti.

## Mtandao wa intaneti

Kama ilivyo kwa kampuni za simu, kama taarifa haijalindwa kiufundi au inalindwa na kanuni za kisheria, mtandao wako wa intaneti utatoa taarifa na ufuatiliaji wa mazungumzo yako. Mtoa huduma wako wa huduma za mtandao wa intaneti anaweza kurekodi na kufuatilia mawasiliano yako. Mwisho wa mitandao kama vile facebook, watoa huduma ya mtandao kwenye jamii kama vituo vya kutoa huduma za intaneti na hoteli ambapo umeunganishwa unakua kwenye hatari ya kuingiliwa.

Hapa ni baadhi ya tahadhari za kuchukua:-

### *Matumizi ya barua pepe iliyolindwa*

Watoa huduma za mfumo wa tovuti, wanaweza kutoa ulinzi kwa kiasi tu. Katika huduma kama vile Gmail za Google au Riseup netuse "transport layer security", au TLS/SSL. Hii ina maana kwamba, wakati kampuni zinaendesha huduma zinaweza kusoma barua pepe zako (Google inatumia hiyo kwa ajili ya kujitangaza matangazo maalumu) vyombo vya kati havina uwezo wa kusafirisha taarifa ndani na nje ya kampuni.

Kuhakisha kwamba huduma unayotumia inalinda mawasiliano yako kutoka vyombo vingine, angalia anuani ya mtandao kwa juu kwenye kisakuzi chako; kama inaanza na "https;//" tofauti na "http://" mawasiliano yako angalau kwa kiasi yamelindwa, na kwa hiyo ni bora ukwepe ufuatiliaji.

Huduma kama twitter, facebook na Microsoft Hotmail sasa zinatoa nafasi bure lakini unaweza kuchagua namna ya kulinda mawasiliano. Unaweza kutafuta nyaraka zao zilizopo kwenye kumbukumbu ya mtandao na kujifunza namna ya kufanya.

**Ujumbe wa papo kwa hapo**

**Barua pepe ya Google inatoa taarifa ya ujumbe wa papo kwa hapo**, bila kuacha kumbukumbu ambayo pia inaziwia mazungumzo kati ya watumiaji wawili. Hii inafanya kazi vizuri pale ambapo watumiaji wote wameiruhusu wakati wa kuwasiliana. Ujumbe wa papo kwa hapo kwenye facebook, yahoo, na kwa wengine sio salama.

**Skype** ni programu nyingine inayofaa kwa ajili ya kulinda mawasiliano ya sauti. Inalinda mawasiliano yake lakini hutumia njia zake kwa siri, hivyo ni vigumu kujua kiwango cha usalama na endapo itakuwa ya ufanisi hapo baadaye.

**Cryp-o-Cat**;- ni programu ya ulinzi wa ujumbe wa papo kwa hapo kwenye mtandao. Ingawa hakuna ushahidi, inatoa kiwango cha usalama na urahisi wa kutumia. Nywila iliyokubalika kutumika kati ya sehemu mbili zinazowasiliana lazima itumiwe.

**Tor**;-ni programu ya bure iliyo wazi, ambayo inaweza kusaidia kulinda kazi ya utafiti wako na vyanzo vingine kwenye mtandao. Ni rahisi kupakua toka kwenye mtandao na inalinda watumiaji wake, kwa kuzuia na kuchanganya taarifa kupitia waunganishaji wanaojitolea kabla ya kupelekwa kwenye mitandao mipana ya intaneti. Angalizo; hata hivyo hiyo inaweza kwenda taratibu na kufungiwa au inakuwa vigumu kupata taarifa katika baadhi ya nchi.

Jitsi Secure Audio, Video and Instant Text Message, ni program iliyowazi inayowezesha kutuma ujumbe wa papo hapo (Instant Messaging – IM), na mazungumzo ya sauti na video kwenye mtandao (voice and video chat). Inawezesha aina nyingi ya mazungumzo yanayotumika sana pamoja na simu ikiwemo SIP. Hutoa maneno yanayoficha habari na jumbe fupi kupitia OTR – Off the Record, na wakati wa mazungumzo ya sauti na video (ZRTP, SRTP)

**Simu za kisasa ni changamoto kuzilinda kwa sababu ya utata wake**

### *Vyombo vya kuwezesha za kupata mafaili.*

Mafaili yaliyofichwa na programu kama vile, windows' BitLocker, Mac's File Vault au the

independent TrueCryptproject, zitaruhusu kuweka nywila kwa ulinzi wa faili husika, akaunti yako au hata mfumo mzima. Taarifa inayo hifadhiwa namna hii haisomeki hata na mtu ambaye anamamlaka ya kompyuta yako. Programu hiyo hiyo inaweza kutumika kwenye flash drive. Hakikisha umechagua nywila iliyo thabiti.

Simu za kisasa ni changamoto kuzilinda kwa sababu ya utata wake. Unaweza penda kufanya uchunguzi kupitia programu ya kutunza taarifa iliyopo sehemu hiyo. Programu ya activism group Mobile Active inatosha kulinda vifaa vya simu.

### *Kuondoa Habari Nyeti*

Kama unahofia mamlaka kuwa inaweza kutaifisha kompyuta yako na unahitaji kufuta kabisa nyaraka nyeti, kwa kubofya futa au kukokota mpaka sehemu ya kutupa nyaraka kama haitatosha. Au unaweza kutumia kompyuta kipengele cha "kufuta kwa kudumu" kama kipo kwenye programu za kompyuta au programu inayopakua mafaili kama vile program ya mtu wa tatu kama vile programu ya Windows Eraser isiyolipiwa.

### *Kuchagua wa nywila thabiti*

Nywila thabiti kwa ajili ya kulinda kwa uhakika ni njia nzuri sana ya usalama wa taarifa zako. Chagua usemi mzuri na wa kipekee, halafu chukua herufi ya kwanza kwa kila neno ndo itakuwa nywila yako.

Kwa mfano, usemi ufuatao: "usalama wa wandishi wa habari ni muhimu sana siku hizi" unaweza leta nywila ifuatayo: "UWWWHNMSSH". Sasa hapo unaweza weka herufi kubwa na ndogo vikichanganywa na vituo mchanganyiko ili kupata nywila fasaha; UWwWHhNMsSH.

---

Kuchagua nywila thabiti, ni muhimu kuwa nazo nyingi kwa kazi zako za kwenye mtandao, ulinzi kwa nywila ni muhimu kulinda vifaa vyako. Hakikisha kuweka nywila kwenye kompyuta yako. Wakati wa semina na wandishi wa habari na wahariri wa Kisumu kuhusu masuala ya ulinzi na usalama, washiriki walijadili mfumo wa matatizo ya mawazo ya "maadui wa ndani". Wandishi wengi kipindi cha semina walielezea hofu yao juu ya wenzao ambao wanafanya kazi ili kukidhi matakwa ya mabwana wa kisiasa au kibiashara wanaowalipa, pia kuwapeleleza kwenye kazi zao. Wandishi wa habari kutoka maeneo mbalimbali ya Kenya wameshuhudia jambo hilo katika mahojiano tofauti. Japo ni ngumu kuficha kazi na taarifa zako zote, ukihakikisha umefunga kompyuta yako kwa nywila thabiti ni hatua muhimu kwa ulinzi na usalama wa kazi zako.

---

# MAMBO YA MSINGI

## Vifaa vya utambulisho wa mwanahabari

Unatakiwa upate vifaa vya utambulisho wa mwanahabari kabla hujaripoti kwa kuwa unaweza ukahitajika kujitambulisha. Waliojiajiri wanatakiwa kupata utambulisho kutoka Baraza la Habari la Kenya na kama ni muhimu, wapate barua kutoka chombo cha habari kinachotoa habari wanazoziandika na kuonyesha uhusiano wao na chombo hicho. Wandishi wa habari wote wanaofanya kazi Kenya wanahitajika kujiandikisha kwenye Baraza la Habari la Kenya. Wandishi wa habari wanaofanya kazi nje ya nchi au kwenye mashirika ya habari ndani ya Kenya wanashauriwa kuomba kibali kutoka chama cha wandishi wa habari Afrika Mashariki (www.fcaea.org), ofisi zao zipo Chester House, barabara ya Koinange, ghorofa ya kwanza.

## Maadili na usalama

Baraza la Habari la Kenya limemechapisha kanuni za mwenendo (www.mediacouncil.ke), imetoa kama muongozo kuwasaidia wandishi wa habari kufanya weledi stahiki. Hii ni muhimu kwa sababu wandishi wana uwezo wa kuwafikia na kushawishi mawazo tofauti tofauti ya watu, anaweza kujenga au kuvunja sifa na takdiri za watu hao



anaoripoti habari zao. Njia zisizo sahihi za uchunguzi, uongo au upendeleo wa kuripoti na kutotenda haki kwenye chanzo au habari ya mhojiwa inapunguza sifa, siyo tu kwa wandishi wa habari ila pia kwenye taasisi ya habari anayoiwakilisha.

Ripoti iliyokosa maadili inaweza kumuweka mwandishi na chanzo husika kwenye hatari na hata kuhatarisha usalama wa taifa. Inaweza pia kupelekea uvamizi dhidi ya vyombo vya habari kwa kukaribisha kashfa na kesi haribifu za madai au hata machafuko kwenye makundi ya kisiasa au vikundi vya wahalifu dhidi ya wandishi ambao wameandika shutuma zisizo na uhakika au kushabikia upande mmoja.

## Usalama eneo la kazi

Changamoto na vitisho kwa wandishi wa habari wa Kenya mara nyingi zinaanzia nyumbani. Ukweli kabisa ni kuwa wandishi, wahariri na waongozaji wanatiwa hatarini na mabwana wanaowalipa kama vile wanasiasa au mashirika, ambao wanatumia "vyanzo vyao" kudhibiti utoaji wa habari. Utafiti wa awali, uliofanywa na jopo kazi cha vyombo vya habari Kenya Mei, 2012, iligundua kuwa asilimia 38 ya wandishi wa habari hawakujali kuripoti matukio ya vitisho dhidi yao, karibu nusu ya wale ambao hawakuripoti matukio, walishindwa kwa kuwa hakuna hatua yoyote iliochukuliwa wakati uliopita, kwa kusikitisha asilimia 27 hawakuripoti vitisho tangu mwajiri wake awe chanzo cha vitisho. Yafuatayo ni maswali ya msingi kujiuliza mwenyewe endapo mwenzako ana mipango mibaya juu yako

Vitu vya msingi vya kutambua usalama mahali pa kazi

Je, kazi niliyopewa sasa, ni nyeti ? Je, kuna watu maarufu, kwenye taarifa hii wenye uwezo wa kuwasiliana na watu kwenye chumba cha habari? Kama jibu ni ndiyo, nani anaweza kuulizwa? Kama jibu ni ndiyo, jiulize maswali yafuatayo:-

1. Kuna mwenzangu au kikundi cha wenzako wanavutiwa na kazi uliyopewa kufanya? Je, mwenzangu au kikundi cha wenzangu wanaonyesha kwa dhati kuwa wanahitaji hiyo nafasi ambayo unayo? Je, mwenzangu au kikundi cha wenzangu wanapeleka taarifa mara kwa mara kwa mtu ninaeandika habari dhidi yake?.

2. Kuna mwenzangu yeyote anaenichungulia kwa karibu pale napokuwa nasoma ujumbe kwenye simu, au naandika barua pepe kwenye kituo changu cha kazi? Kuna mtu yeyote ambaye anatumia muda mrefu kuwa karibu yangu badala ya kwenda

**Ripoti iliyokosa maadili inaweza kumuweka mwandishi na chanzo husika kwenye hatari**

kufanya kazi zake?

3. Kuna mwenzangu anayeonekana kuwa na urafiki na mhariri, muongozaji au mmiliki wa chombo cha habari? Je, wanatumia muda mwingi kujadili ofisini? Je, ni wa kabila moja na kimakusudi wanaongea kwa lugha yao wakijua kuwa wenzao ndani hamuelewi wanachozungumza?

Kama jibu ni ndiyo kwa maswali haya, ni muhimu kujilinda wewe na kazi yako.

- Endelea kuwa na ukaribu na mwenzako uliye na mashaka nae au hicho kikundi lakini hakikisha hutoi maendeleo yoyote ya kazi unayofanya na jaribu kubadilisha mazungumzo yako, uzungumzie maeneo ambayo siyo nyeti ya kazi unayofanya sasa.
- Kama unahofia madhara, endapo utatoa hiyo taarifa kwa wenzako au kikundi unachohofia, kaa nayo kwanza na endelea na majukumu mengine kwa muda fulani.
- Ikionekana kama habari yako haitaweza kuchapishwa tena kwa sababu ya maslahi binafsi ya wachapishaji. Jaribu kutafuta vyombo vingine vinavyotoa habari vinavyoweza kukubali kuchapisha/ kutangaza bila kutoa jina lako.

Wakati ukitambua kwamba kuwa na mashaka na hofu dhidi ya mfanyakazi mwenzako si vyema, kuweka vitu vya msingi vilivyotajwa hapo juu akilini vitakusaidia kukulinda wewe na kazi yako. Kushirikishana na kushirikiana na wenzako ni kitu muhimu-lakini kumbuka mtu unaemshirikisha habari na pia ni muhimu kufahamu kama kunaweza kuwa na maslahi binafsi kwa habari hii ndani ya chumba cha habari.

## Kufanya kazi na vyombo vya habari vya nchi za nje.

Wandishi wa habari mara nyingi wanawasaidia wandishi wa kimataifa kutafuta namna wanavyoweza kuunganisha habari maalumu nchini. Mara nyingine wanawaomba kufanya kazi ya ukalimani. Hii inaweza kuonekana kuwa hatua ya busara kiusalama. Hata hivyo kwa kazi zao, wanashauriwa kupata uelewa halisi wa madhara ya kuchukuwa kazi hizo. Hakikisha kwanza unajielewa wewe ni nani, na kutambua wapi unaelekea. Zingatia jinsi utakavyochukuliwa ukionekana kwenye mazingira ya kigeni tofauti na alivyo mwandishi wa nchi hiyo, kwa kuwa unaweza onekana kama adui. Kuandika habari katika kambi ya wakimbizi ya Dadaab kutoka kwa wandishi wa habari wa mataifa ya magharibi nchini Somalia, inaweza kukuletea matatizo kutokana na utakavyochukuliwa na wanamgambo wenye msimamo  mkali wa Somalia.

Ukielewa unaweza kuikataa kazi fulani, na kuelewa kwa kiwango gani kunasaidia kuwagawa wandishi au watoa habari, pia wanaweza kukusaidia kama utapatwa na matatizo. Pata uelewa halisi wa majukumu yako katika kazi. Je, wewe umeombwa kuwa mkalimani au kutoa huduma za kuongoza?Au pia unatoa taarifa? Ya mwisho ina maana ya nyongeza ya kiulinzi unaopaswa kuufahamu.

## Waendesha blogu na Wanahabari Hadhira

Vyombo huru kama waendesha blogu, wapiga picha za video na wandishi wa habari wa Citzen au Netzen kama wanavojiita wakati mwingine, wametokea kuwa watoaji muhimu wa habari, hasa kwenye sehemu nyeti kama vile uchaguzi mkuu machi 4, 2013 na habari za uvamizi wa kigaidi Westgate Mall Septemba 2013. Vyombo huru vinapokuwa vinafanya kazi ya uandinshi kipindi cha migogoro, inabidi kuelewa athari za kufanya kazi pekee yako bila kuwa na msaada wa taasisi. Mipango madhubuti ya usalama, ikiwemo matumizi ya mawasiliano na vitendo vya mawasiliano ya kila siku ya wanahabari wenzako na ndugu, ni muhimu. Waendesha blogu wanashauriwa kujiunga na chama cha wenye blogu wa Kenya, Kenya Association of Bloggers (BAKE)- http://bake.co.ke ili kuisaidia katika ulinzi wa taasisi.

# WEWE NA NYUMBANI KWAKO: KUWEKA FAMILIA SALAMA



## Mambo yako ya kiafya

Kama ukipewa majukumu mahali ambapo ni mbali na sehemu unayoishi kwa kipindi chochote, utambue madhara ya afya yako na ujiandae kiuhakika hata kama ni amri kutoka kwa mhariri wako.

**tambua madhara ya afya yako na ujiandae kwa makini**

Mwanzoni mwa miaka ya tisini, wakati Tume ya Kuchunguza kifo cha Dkt. Robert Ouko, ambaye alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, vyombo vikubwa vya habari viliwapeleka wandishi wao waliobobea kutoa taarifa juu ya tukio hilo. Kwa bahati mbaya, watu hawa waliopewa jukumu gumu la kutafuta habari hawakuwa wamejiandaa ipasavyo. Huku wakiwa salama kwenye ofisi zao zenye viyoyozi Nairobi, wahariri hawakutambua kabisa ukubwa wa changamoto za kutafuta habari mjini Kisumu na awali walikataa kuongeza posho za wandishi, ambazo zitawafanya watekeleze majukumu yao kwa hali nzuri. Uhalisia wa hali ulibadilika pale wandishi walipoanza kuugua.

## Usalama wa familia

Hakuna hofu kubwa kama kujua kuwa familia yako ipo kwenye hatari. Kuzitafuta sababu zinazo hatarisha familia yako inaweza kuongozwa na tabia za maadui zilizopita.

Tahadhari za kuchukua.

- Utambue mambo yako au mtu yeyote kwenye familia aliyerusha habari kwenye mitandao ya kijamii kama vile facebook. Wale wanaotaka kukutisha, hupenda kuchunguza vitu vyako kwenye mtandao.
- Epuka kushirikishana sana kwenye mambo ya kazi na familia. Mwana familia ambaye hana taarifa kuhusu kazi yako ya upelelezi, hii ni mantiki ambayo haitalenga mvamizi anaehitaji taarifa kwa kushinikiza.
- Hakikisha watoto wako wapo kwenye uangalizi muda wote.
- Acha kazi kwa kitambo kidogo, ikiwezekana safiri sehemu nyingine kwa muda.

## Baada ya majukumu/kazi.

i) Toa maelezo kabla ya kazi.

ii) Kuandika na kutoa taarifa. (tazama kiambatisho II)

iii) Kumudu kiwewe na mfadhaiko.

### *Maelezo kabla ya kazi.*

Hiki ni kipengele muhimu kwa hatua yoyote ya kiusalama kwa kuwa inasaidia pande zilizoshiriki kujipanga kiulinzi kutokana na walichojifunza. Kiujumla inatakiwa iwe kamilifu na makini, imuweke mwandishi tayari zaidi. Malengo ni kupata kadiri iwezekanavyo picha halisi ya kazi ilivyofanyika, changamoto walizopata, kama zipo, namna ambavyo walikabiliana nazo, sehemu yoyote ambayo haikupitiwa wakati wa mipango na hali yeyote ya dhiki na kutisha miongoni mwa taarifa zingine.

## *Matokeo ya Mfadhaiko*

Hali kufadhaika baada ya kiwewe na msongo ni hali ya kawaida kwenye matukio yasiyo ya kawaida. Msongo au dhiki haiwadhuru wapiganaji pekee ila pia wandishi wa habari wa eneo hilo wanaweza pata matatizo yanayopelekea maumivu au kupoteza maisha.

Hali ya kufadhaika baada ya kiwewe na msongo, inaweza kujionyesha kwa njia tofauti. Mtu anayepata mfadhaiko anaweza kosa kuhusiana na kitu chochote, na tofauti nao huwaza tu kuwa hapa kuna kitu ambacho siyo sahihi au kitu cha ziada anachohitaji kufanya. Kwa wandishi wa habari ambao kazi yao ni kuangalia na kuripoti matukio, na bila kuchukua hatua, kutazama maafa kwa binadamu kunawafanya washindwe kuzuia hisia zao. Wandishi ambao wanawahoji wahanga wa kiwewe, kiukweli, wao wenyewe wanajiweka kwenye mazingira ambayo wataalamu wanaita kiwewe kwa niaba ya waathirika. Wahariri wa picha na video wanaweza kuathirika kutokana na kujishughulisha na picha hizo zenye tukio moja na jingine.



Ishara za mfadhaiko.

- Kwa muda mrefu kuwa mtu mwenye wasiwasi, mwenye hasira, mwenye huzuni na hasira.
- Matatizo ya kula au kupata usingizi.
- Mapigo ya moyo kwenda mbio, kutokwa na jasho, kuwa na hofu, kichwa kuuma, kichefu chefu na maumivu ya kifua.
- Kuwa na mahusiano yasiyoridhisha kazini.
- Kuacha kazi mara kwa mara bila kuwa na sababu za kueleweka.
- Kukazania kazi ya mwenzako kusiko kwa kawaida.
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya.

Hali ya mfadhaiko baada ya kiwewe na msongo, inaweza kukaa kwa miezi kadhaa, kama isipotibiwa inaweza kuleta madhara mengine ya kiafya, kwa mfano; kusababisha shinikizo la damu.

## Njia za kujihadhari

Kutambua kuwa umepata kiwewe au maumivu ni hatua ngumu. Wandishi wengi wa habari na wanajeshi hua wanavitu wanavyovifanya kutokana na mazingira na ya makundi yote, ili kujiwezesha kutambua madhara ya athari hizo.

Wandishi wanahitaji kujifunza jinsi ya kuchukua tahadhari. Kwa ufupi kuchukua likizo inaweza ikafaa. Hivyo anaweza kutafuta ujasiri wa kumwambia mhariri kuwa anahitaji pumziko. Muhimu zaidi kujipa nafasi ya kuomboleza au vinginevyo uzitawale hisia zako. Wataalamu wanasema mazoezi ya mara kwa mara yanasaidia kupunguza msongo wa mawazo.

Kuzitawala hisia zako ni njia mojawapo ya kupunguza msongo. Wandishi wanaweza kufaidika kutokana na majadiliano ya uzoefu wa kila mmoja. Sehemu ambayo hili linaweza kufanyika, inaweza kuwa chumba cha habari au sehemu ya karibu yenye mkahawa. Kiongozi wa chumba cha habari inabidi asaidie kuandaa nafasi na vikao vya wandishi kwa ajili ya mazungumzo.

Kuzungumza na watoa ushauri nasaha wengine ni njia nyingine kwa wandishi wa habari kuzitawala hisia zao. Wataalamu wa kutoa ushauri wana uzoefu wa kuwatibu watu wenye matatizo hayo, na wanapendekeza kuwa, rafiki yako ni sehemu nzuri ya kuanzia kupata ushauri. Rasilimali muhimu kwa wale wanaosononeka na athari/machafuko Kenya inajumuisha kituo cha wahanga na mateso-www.cvt.org.

www.kenyalaw.org/Downloads/TheConstitutionKenya.pdf

# Kiambatanisho cha I: Kutathmini Hali ya Usalama Kabla ya Kwenda Kazini

Kigezo hiki kimetolewa kama mwongozo. Fahamu kwamba kila mwanahabari au shirika la habari hukumbwa na hali tofauti inayohitaji kigezo hiki kufanyiwa mabadiliko.

1. MAELEZO YA KAZI: Tambua tarehe ya kusafiri, utaratibu wa safari, na majina ya wafanyakazi wenza, wanahabari huria, na watu wengine utakaoshirikiana nao.

2. TATHMINI YA HATARI: Tambua hatari inayoweza kutokea.

2.1 WATU HASIMU: Chunguza kama kuna uwezekano wa wewe, kundi lako, au washiriki wako kuweza kulengwa ili kufanyiwa ujasusi au kushambuliwa.

Tambua watu wanaoweza kuwa mahasimu wakiwemo watu wenye mamlaka serikalini, wahalifu, waasi, na makundi yaliyoharamishwa.

2.2 HATARI KATIKA ENEO: Tambua hatari zinazohusishwa na kazi ya uanahabari katika eneo fulani. Hatari kama hizo zinaweza kuwa ni pamoja na kutokea kwa ghasia/ongezeko la ghasia; utekaji nyara; kujipata ukiwa na maafisa hasimu (matatizo ya kuvuka mipaka, kutiwa mbaroni, kutiwa kizuizini); kuchunguzwa na watu au kwa njia ya elektroniki, n.k.

2.3 USALAMA KWA WENYEJI WAKO: Tambua hatari kwa wenyeji wako unaoshirikiana nao (wafasiri, madereva, waleta habari, mashahidi, n.k.)

2.4 CHUNGUZA HATARI: Shughulikia hatari hasa zinazokabili kazi yako. Kwa mfano: unapohoji, unapopiga picha, unaporekodi video, unapotembelea mahali, unapopata au unapobeba nyaraka na picha zenye ushahidi).

2.5 SIFA ZAKO: Eleza namna sifa zako, sifa za wenzako, na sifa za chombo chako cha habari zinaweza kukuongezea au kukupunguzia hatari.

2.6 MIKAKATI INAYOPENDEKEZWA YA KUPUNGUZA HATARI: Fafanua mikakati utakayochukua wewe, kundi lako, makao makuu, na watu wengine ili kupunguza hatari inayotokana na kazi yako.

2.7 MALAZI: Fahamu hoteli zote, vyumba vya kukodi, nyumba za watu binafsi, na aina zingine za malazi ambamo unaweza kulala katika sehemu zote utakazotembelea. Eleza kwa nini lojinii unayopendekeza ni salama. Toa maelezo kuhusu namna utakavyowasiliana na wenyeji wa malazi yako.

2.8 MIPANGO YA USAFIRI: Eleza kuhusu mipango ya usafiri.

2.9 MAWASILIANO: Eleza ikiwa wewe na kundi lako mtatumia simu ya rununu ya kimataifa, simu za nchini, simu za setilaiti, simu zilizounganishwa kwa nyaya, redio zinazobebwa mkononi, na utoe maelezo kuhusu changamoto zinazoambatana na matumizi ya kila chombo. Taja ikiwa kundi litapata mtandao wa intanetu wakati wote.

3. AINA YA UHUDUMU: Eleza ikiwa wewe au kundi lako mnapanga kufanya kazi kama watu mashuhuri au watu wa daraja la chini na mikakati itakayoshughulikia hatari zinazoambatana na kila kiwango. Eleza jinsi wewe na kundi lako mtakavyoingia kwenye nchi na mtakavyojitambulisha katika hali tofauti (mpakani, kwenye vituo vya ukaguzi, na mnapokutana na maafisa wa serikali).

3.1 UTAFITI NA SHUGHULI ZINGINE: Eleza jinsi wewe na kundi lako mnavyopanga kufanya kazi ya wanahabari kwa njia iliyo salama kwako na kwa wale unaohusisha. Ikiwezekana, taja ikiwa mikakati maalumuu itachukuliwa kuficha utambulisho wa watu fulani na ni njia gani itakayotumiwa kuwasiliana na watu ili kuepuka kufichua utambulisho.

3.2 KULINDA HABARI: Eleza mikakati maalumuuu ya kulinda habari nyeti ukiwa kazini. Taja ikiwa wewe au kundi lako mtatumia vifaa vya kielektroniki kukusanya na kuhifadhi habari (kinasa sauti, kamera, kompyuta, n.k.) na mikakati itakayohakikisha usalama wa habari ikiwa kifaa kitachukuliwa au kufikiwa na mtu mwingine.

3.3 UTARATIBU WA KUINGIA MAHALI: Eleza kuhusu utaratibu wa kuingia kazini. Taja mwenyeji wako wakati wa kuingia mahali; kawaida na nyakati za mawasiliano; na njia ya mawasiliano.

3.4 Utaratibu wa kuchukua hatua ikiwa kundi lako halitaweza kuingia mahali.

Fafanua:

- Ikiwa kuna mshiriki aliye na jukumu la kupokea watu wanaoingia, na ni wakati gani anafaa kujulisha wasimamizi;
- Ikiwa na shirika la habari linafaa kuwasiliana na watu walio nyanjani kwa dharura na litafanya hivyo lini;
- Ni hatua gani za ziada inafaa kuchukuliwa au kukosa kuchukuliwa na shirika la habari (hatua zinaweza kujumuisha kujulisha jamaa, kujulisha wanahabari wengine, au kuwasiliana na ubalozi).

3.5 MAWASILIANO: Toa habari kuhusu mawasiliano (nambari za simu ya rununu na simu ya waya, barua pepe) ya watu wafuatao:

- Wafanyakazi wanaosafiri kwenda kazini
- Wafanyakazi wanaopokea watu wanaowasili
- Wasimamizi na watu wengine wanaoweza kufikiwa katika makao makuu
- Washiriki wasiokuwa wafanyakazi (washauri, wafasiri, madereva)

6. MAWASILIANO YA DHARURA:

Mawasiliano ndani ya nchi (a) taja mtu aliyechaguliwa kuangazia suala la usalama nchini (kwa mfano mfanyakazi mwenza aliyechaguliwa na anayeaminika) atakayefahamishwa kila wakati kuhusu mipango yenu, safari zenu, na mahali mlipo; (b) toa orodha ya majina zaidi ya watu walio nchini ambao watatoa usaidizi ikiwa kuna tisho la usalama, au hali nyingine ya dharura.

## *Kutoa jibu*

Baada ya kutathmini hatari na vitisho, kwa kujaza jedwali la usalama, sharti uandae mkakati wa kushughulikia kila hatari.

Unaweza ukatumia njia zifuatazo:

- Kukubali kuwepo kwa vitisho kwa sababu unaona unaweza kuishi nazo.
- Kupunguza hatari kwa kushughulikia vitisho na uwezekano wa kuvamiwa.
- Kushughulikia vitisho kwa ushirikiano na wanahabari wengine au mashirika mengine ili kupunguza hatari kutokea.
- Kujiepusha na hatari kwa kubadili au kuacha unachofanya au kubadilisha njia unayotumia ili kupunguza kutokea kwa hatari.

Mojawapo ya sehemu kwenye mfumo huu ni kutambua mtandao wa umoja. Ni watu gani au mashirika gani ambayo wanahabari wanaweza kuwasiliana nao ikiwa kuna dharura? Ikihitajika, ni nani anaweza kutoa mchango kwa itifaki ya usalama? Je, inawezekana kutambua mtu anaweza kutumika miongoni mwa wafanyakazi wenza, familia au marafiki? Mara nyingi ni bora kutumia mchanganyiko wa mbinu tofauti . Ukiona kuwa unahitaji usaidizi kufanya hivi, basi kumbuka kuwa mashirika ya humu nchini na yale ya kimataifa yanayosaidia wanahabari hutoa usaidizi.

# Kiambatisho II: Kuripoti Kisa cha Usalama na Tisho

| | | |
|---|---|---|
| **Aina ya tukio**: shambulizi dhidi ya mtu, kukutana na watu hasimu, kunyanyaswa, kupata simu au jumbe za vitisho, kuchunguzwa, kunyang'anywa vifaa vya kazi, vifaa kuharibiwa, kukatazwa kufika mahali kwenye habari, kutiwa mbaroni, kuibiwa, kutekwa nyara, kutukanwa, kupekuliwa huku ukishikwa shikwa visivyo, dhuluma za kimapenzi, na kusumbuliwa kwa ujumla, n.k. (Tafadhali fafanua): | | |
| **Tarehe na Wakati wa tukio:** | | |
| **Mahali tukio lilitokea: (taja mahali penyewe):** | | |
| **Utambulisho wa waliohusika na maelezo ya gari, ikiwa yapo:** | | |
| **Mashahidi (jina na njia ya mawasiliano)** | | |
| **Maelezo kuhusu tukio, orodhesha kama ilivyotokea:** | | |
| **Hatua iliyochukuliwa (ulifanya nini papo hapo?):** | | |
| **Ni usaidizi gani unatakikana: (usaidizi kwa familia, ushauri nasaha, uchunguzi zaidi, kuhamishwa, n.k. – fafanua):** | | |
| **Jina kamili:** | **Tarehe:** | |
| **Jina la shirika la habari linalohusika kwa kazi ile:** | | |
| **Kwa Matumizi Rasmi**<br><br>1. Mapendekezo ya kwanza:<br><br>2. Je, tukio linaonyesha mwenendo wa tabia?<br><br>3. Taja jina la mtu aliyepewa jukumu la kufuatilia na muda maalumuu wa kufanya kazi. | | |

# Kiambatisho III: Chombo cha kutathmini hatari na mikakati ya usalama

Mwongozo Mpya wa Ulinzi wa Watetezi wa Haki za Binadamu wa Protection International unatoa taratibu zifuatazo, zinazoweza kutumiwa na wanahabari wanapotathmini hatari wakiwa katika kazi yenye hatari. Miongozo iliyotolewa hapo chini imeandikwa kama maswali na imeambatanishwa na hali kwa mhariri na mwanahabari kupitia mchakato muhimu wa kupanga.

- Je, mazingira ya kisiasa na kijamii ni salama kwa kazi ya uanahabari?
- Ni mambo gani hasa yanayoweza kuleta ukosefu wa usalama katika sehemu tunayofanya kazi?
- Ni wadau gani hasa au makundi yanayohusika na mambo haya?
- Kazi yetu itaathiri vipi mambo haya, iwe ni kwa uzuri au kwa ubaya?
- Tutajibu au tutaonyesha hisia zipi tukiwindwa na watu hawa au wafuasi wao kwa sababu ya kazi yetu?
- Je, mashirika yetu ya habari na wanahabari wenzetu wanapokelewa vipi kazi sehemu wanayofanyia kazi?
- Wanahabari wetu wamefanya kazi aje katika sehemu hizi hapo awali? Au kwa mambo yaliyotokea kabla ya kazi hii na yanahusu mkakati wetu wa usalama?

Ukisoma kwa makini, utaona kwamba maswali haya yatakusaidia kutathmini matishio ya usalama wako, pamoja na uwezekano wa wewe kutishwa pamoja na uwezo wako.

## SEHEMU YA KWANZA: Kutathmini hatari

***Kaunti:***

***Nchi:***

***Kazi yenyewe:***

***Mhariri anayesimamia kazi:***

***Tarehe:***

1. Maelezo ya kazi:
2. Mpango wa kazi na ratiba ya safari:
3. Maelezo ya mawasiliano ya walio kwenye kikundi na jamaa wa karibu:
4. Maelezo ya nyuma:
5. Taja mambo yoyote yanayotishia usalama katika eneo la kazi:

## SEHEMU YA PILI: Mikakati ya Usalama

6. Wajibu wa majukumu ya walio kwenye kikundi:
7. Mikakati ya ulinzi iliyowekwa:
    - Uhusiano na maafisa wa serikali:
    - Mipango ya usafiri:
    - Bima:
    - Bima ya matibabu:
    - Vifaa muhimu kama vile vya huduma ya kwanza:
    - Vifaa vya uanahabari:
    - Vifaa vya kujilinda kwa usalama wako binafsi:
    - Usalama wa habari (diski ya kuhifadhi, n.k.):

8. Maelezo ya mawasiliano na watu nyanjani:

9. Mipango ya usafiri, mahali pa kuishi na usafiri:

10. Mpango wa kuhamishwa panapotokea hatari:

11. Kupanga kuwa tayari kwa jambo lolote:

12. Thibitisha kuwa huduma muhimu ziko na zinaweza kupatikana katika sehemu mnayofanya kazi kama vile hospitalini, vituo vya polisi, mahala salama pa kuishi, utunzaji wa gari au gereji, vituo vya mafuta, n.k.

# MAONI

Madhumuni ya mwongozo huu ni kuwapa wandishi na vyombo vya habari maarifa ya ziada (vidokezo) na baadhi ya zana ambazo zinaweza kuwa na manufaa katika kuboresha ulinzi na usalama wao. Hii ni miongozo muhimu kwa ajili ya ulinzi na usalama kwa ujumla, na inatarajiwa kwamba kutumika kwao nchini Kenya, kutapelekea kuweka mazingira ya kazi yaliyo salama kwa wandishi wa habari. Hatimaye, usalama ni jukumu la kila mtu na sote tuna wajibu wa kuwalinda wengine na kujilinda wenyewe.

Mwongozo ni ishara ya kuwa na mwelekeo mpya katika uendeshaji wa kazi ya uandishi wa habari. Kwa kiasi kikubwa mwongozo huu umenufaishwa na miongozo mingine inayotumika duniani pamoja na ujuzi wa wanataaluma wa uandishi wa habari wa ndani ya nchi. Mwongozo huu unaongozwa na ukweli kwamba kuwepo kwa vitisho au mashambulizi dhidi ya wandishi wa habari siyo hali inayotokea katika eneo moja tu duniani, bali kuna tofauti baina ya maeneo yote katika idadi na makali ya hayo matukio. Hivyo, miongozo ya aina hii huwa inafana katika muundo, maudhui, mtazamo na msukumo.

Mwongozo huu unajaribu kutoa muktadha wa nchini ili kuweza kushughulikia mambo ambayo yanahusu mazingira ya kipekee ya Kenya. Ingawa hatua za dhati zimechukuliwa ili kuufanya huu mwongozo uwe wa kina, kuna uwezekano kwamba mwongozo haujaweza kuzingatia hatari au athari zote. Kwa hivyo, kuna fursa ya kufanya utafiti zaidi ili kuimarisha hati hii.